

**MKABALA UNAOTUMIKA KATIKA UTUNGAJI WA MITIHANI YA  
KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI: Mfano Chuo Kikuu Cha Taifa Cha  
Zanzibar**

**Makame Sheha Mgasho**

**Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa  
Wazungumzaji wa Lugha Nyingine (M.ED. TEKSOL)**

**CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR**

**Disemba, 2020**

**MKABALA UNAOTUMIKA KATIKA UTUNGAJI WA MITIHANI YA  
KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI: Mfano Chuo Kikuu Cha Taifa Cha  
Zanzibar**

**Na**

**Makame Sheha Mgasho**

**METK/2/2018/03/TZ**

**Tasnifu Inayowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Sehemu ya Masharti ya  
Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wazungumzaji  
wa Lugha nyingine (M. ED. TEKSOL)**

**Skuli ya Elimu**

**CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR**

**Disemba, 2020**

**ITHIBATI**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii yenye mada: *Mkabala Unaotumika katika Utungaji wa Mitihani ya Kiswahili Kama Lugha ya Kigeni: Mfano Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar* na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kwa ajili ya utahini wa Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wazungumzaji wa Lugha Nyingine ya Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

.....

**DKT: Haroun A. Maalim**

**Skuli ya Elimu**

**CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR**

**Disemba, 2020**

**TAMKO**

Mimi, **Makame Sheha Mgasho**, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutunikiwa shahada kama hii au shahada nyingine yeyote.

.....

**Makame Sheha Mgasho**

**METK/2/2018/03/TZ**

**Disemba, 2020**

**HAKIMILIKI**

Tasnifu hii inalindwa na sheria za haki miliki za kitaifa na kimataifa. Hairuhusiwi kwa namna yeyote ile kunakili kazi yote au sehemu ya kazi hii bila ya idhini ya maandishi ya mwandishi au Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar isipokuwa kutumia sehemu ndogo kwa lengo la utafiti au kujisomea au kufanya uchambuzi yakinifu wa kitaaluma.

## SHUKURANI

Kabla ya yote nachukuwa nafasi hii kumshukuru Allah (S.W) kwa kunijaalia uhai na afya njema, uwezo, fikra, nguvu, hamu, ari, ustahamilivu na uvumilivu mkubwa katika kuhakikisha kwamba naikamilisha na kuifanikisha kazi hii katika hali ya ubora mkubwa. Kwani bila ya uwezo wake Mwenyezi Mungu hakuna linalowezezana, pamoja na hayo, pia ninamtakia rehema na amani kipenzi chake bwana Mtume Muhammad (S.A.W).

Nimelazimika kuyafanya hayo kwani iwapo sitoshukuru, kwa njia moja au nyingine sitokuwa na fadhila, pia kipimo cha utu na ubinaadamu wangu kitakuwa na mapungufu. Sirahisi kuwataja wote waliotoa michango na ushauri juu ya kuufanikisha utafiti huu. Ila waamini kuwa michango na ushauri wao vimepokelewa kwa moyo mkunjufu, na ninawaombea kwa Allah awajaze imani na moyo wa kutowa michango yao katika shughuli nyingine za kimaendeleo na kitaaluma, pia awape afya njema na awajaalie baraka katika kazi na maisha yao ya kila siku, AMIN.

Aidha ninapenda kumshukuru kwa dhati mwalimu wangu na msimamizi wa utafiti huu Daktari Haroun A. Maalim. Daktari Haroun kwa ukamilifu kabisa alikubali kuisimamia kazi hii ya kitaaluma hakuacha kunishauri tangu nilipowasilisha pendekezo langu la utafiti huu, hadi katika hatua ya uwasilishaji wa tasnifu hii. Alikuwa na mimi kwa ukaribu mkubwa katika kuniongoza, kunielekeza, kunikosa na kunijenga moyo wa ustahamilivu na uvulivu katika mchakato mzima wa kuitaarisha kazi hii. Wakati akiyatekeleza hayo kwangu hekma na busara kubwa vilimtawala kwa kadri Allah alivyomuwezesha na hakisita kunipatia msaada pale nilipouhitaji. Napenda kusema

kuwa nimejifunza mengi mazuri kutoka kwake, kwani nimeweza kukuza uelewa wangu katika nyanja ya utafiti, bila ya shaka hali hiyo imeniongezea ujuzi wa kutatua matatizo mengi ya kiutafiti na kitaaluma. Jitihada zake za usimamizi kwangu siwezi kuzimaliza ila namuomba Allah (S.W) amzidishie uhai, uwezo, nguvu, ujasiri, afya njema na mafanikio katika kazi zake za kitaaluma na kijamii katika maisha yake ya kila siku. Kama kuna jambo la kujivunia kutoka kwa msimamizi wangu, ni kunijenga moyo wa kufanya kazi katika mazingira ya *uvumilivu, ujasirina kujituma* muda wote.

Sambamba na hayo nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mke wangu Kipenzi Salma Khamis Suleiman kwa kunivumilia na kunisitahamia katika kipindi chote cha masomo yangu kwani kwa hakika ulikuwa ni wakati mgumu sana kwake Allah amlipe kila la kheri kwa ushujaa huo aliounesha katika kipindi hicho kizito.

Aidha, napenda kumshukuru Daktari Zainab Ali Iddi wa Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kwa kunipa ushauri na mawazo ambayo yaliweza kunisaidia kuisoma na kuihitimi kozi hii ya Ufundishaji Kiswahili Kwa Wazungumzaji wa Lugha Nyingine katika ngazi hii ya Shahada ya Uzamili.

Kwa heshima ya kipekee napenda kuwashuku walimu na wafanyakazi wote wa kitivo cha Kiswahili kwa Wageni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kwa kunipatia mashirikiano mazuri ya kitaaluma pamoja na walimu wangu walionipa mafunzo ya kozi hii, akiwemo Prof. Alwiya S. Omar, Daktari Haroun A. Maalim, Daktari Zainab Ali Iddi, Daktari Muhamed S. Khatib, Daktari Arnold B. G. Msigwa, Daktari Maryam J. Ismail na Mwalimu Said S. Khamis ewe Mwenyezi Mungu ninakuomba uwape maisha

marefu yenye afya njema ili waweze kuwasomesha wataalamu wengine wa kufundisha kozi hii ya Ufundisha Kiswahili kwa Wazungumzaji wa Lugha Nyingine.

Mwisho kabisa natoa shukrani zangu za dhati, kwa wanafunzi wenzangu na Mkurugenzi wa Masomo ya Juu na Utafiti Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kwa mashirikiano yao mazuri walionipatia wakati wote wa kujifunza. Namuomba Allah awabariki wote kwa ujumla na awape siha njema**AMIN**.Kwa kumalizia naomba ifahamike kwamba udhaifu wowote utakaonekana katika kazi hii ni udhaifu wa mtafiti na sio wa watoa taarifa.



**TABARUKU**

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa **Kininga Nema Hamid** na almarhum **Sheha Mgasho Sheha** kwa kunipatia malezi bora yenye kuzingatia misingi ya Dini ya Kiislamu pamoja na kujitolea kwa hali na mali katika kuhakikisha kwamba mtoto wao anapata makuzi mazuri. Huku wakizingatia kwamba wanamuwekea misingi imara ya maisha kwa kumpatia elimu yenye uwezo wa kumuongoza katika harakati za kila siku pamoja na kumuwezesha kuwa na maandalizi mazuri ya kesho akhera twendako. Kiukweli hakuna cha kuwalipa isipokuwa ni kusema *Ahsante* na Allah (S.W) awape mwisho mwema na akawaingize katika pepo ya Firdausi. **AMIN.**

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu Mkabala Unaotumika Katika Utungaji wa Mitihani ya Kiswahili Kama Lugha ya Kigeni: Mfano Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi matatu. Kwanza kufafanua kiasi gani walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni wanavyoifahamu mikabala ya utungaji mitihani. Pilikubainisha aina ya mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni. Tatu kuchunguza mtazamo wa walimu juu ya mkabala wanaotumia zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni. Utafiti huu ulifanywa katika Idara ya Kiswahili kwa Wageni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ilikuwa Nadhari ya Tabia ya Umoja (Unitary Trait Hypothesis) kama ilivyoasisiwa na Oller (1979). Misingi mikuu ya nadharia hii ni kuipima lugha kwa njia ya mjumishi pamoja na uzingatiaji wa mazingira halisi ya watumiaji wa lugha inayohusika wakati wa upimwaji wake. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni walimu saba wanaosomesha Kiswahili kwa wageni, watoa taarifa hao walipatikana kwa usampulishaji tajwa. Mbinu zilizotumika ni mbinu ya dodoso kwa ajili ya kukusanya data za lengo la kwanza hadilengo la tatu, na mbinu ya uchambuzi wa nyaraka ilitumika kwa ajili ya kukusanya data za lengo la pili tu la utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yalieleza kwamba walimu wanaosomesha Kiswahili kwa wageni wanaofahamuwa mikabala ya utungaji mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa asilimia 57%. Pia utafiti ulionesha kwamba mkabala unaopima stadi nyingi za lugha kwa wakati mmoja ndio ambao hutumika zaidi, na mtazamo wa walimu kuhusu mkabala unaotumika zaidikwamujibu wa matokeo ya utafiti ni wenye kufaa kwani unawapatia matokeo wanayoyahitaji katika upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Utafiti huu ulitoa mapendekezo ya kwamba walimu waongeze taaluma yao juu ya mikabala ya upimaji, pamoja na uzingatiaji wa stadi zote kuunne za lugha katika upimaji wa wanafunzi ili kuhakikisha kwamba hakuna stadi ya lugha hata moja ambayo inaachwa nyuma wakati wa upimaji wa wanafunzi.

## YALIYOMO

ITHIBATI .....	2
TAMKO .....	ii
HAKIMILIKI .....	iii
SHUKURANI .....	iv
TABARUKU .....	vii
IKISIRI.....	viii
YALIYOMO .....	ix
ORODHA YA MAJADWELI .....	xiv
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	<b>1</b>
UTANGULIZI .....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Utafiti.....	1
1.3 Tatizo la Utafiti .....	2
1.4 Malengo ya Utafiti .....	3
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti .....	3
1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti.....	3
1.5 Maswali ya Utafiti.....	4
1.6 Umuhimu wa Utafiti .....	4
1.7 Mawanda ya Utafiti.....	5

1.8 Hitimisho.....	6
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>7</b>
MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA.....	7
2. 1 Utangulizi.....	7
2.2 Mapitio ya Maandiko .....	7
2.2.1 Ufahamu wa Walimu Juu ya Mikabala ya Mitihani .....	7
2.2.2 Mkabala Unaotumika Zaidi Katika Utungaji wa Mitihani .....	11
2.2.3 Mtazamo wa Walimu Kuhusu Mkabala Unaotumika Zaidi katika Upimaji.....	15
2.3 Pengo la Utafiti .....	17
2.4 Kiunzi Cha Nadharia.....	18
2.5 Hitimisho.....	20
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>21</b>
MBINU ZA UTAFITI .....	21
3.1 Utangulizi.....	21
3.2 Mkabala wa Utafiti.....	21
3.3 Eneo la Utafiti .....	22
3.4 Watoa Taarifa, Sampuli na Usampulishaji.....	23
3.4.1 Watoa Taarifa.....	23
3.4.2 Sampuli .....	23
3.4.3 Usampulishaji.....	24
3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	25

3.5.1 Mbinu ya Dodoso.....	25
3.5.2 Mbinu ya Uchambuzi wa Nyaraka.....	26
3.6 Zana za Ukusanyaji wa Data.....	27
3.6.1 Orodha Hakiki.....	27
3.7 Uchambuzi wa Data.....	27
3.8 Maadili ya Utafiti.....	28
3.9 Uaminikaji wa Data.....	28
3.10 Hitimisho.....	30
<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>31</b>
<b>UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....</b>	<b>31</b>
4.1 Utangulizi.....	31
4.2 Ufahamu wa Walimu Juu ya Mikabala ya Utungaji Maswali ya Mitihani.....	31
4.2.1 Uelewa Juu ya Maana ya Mikabala.....	32
4.2.2 Kutaja Aina za Mikabala.....	34
4.2.3 Kuorodhesha Aina za Mikabala.....	35
4.2.4 Uwiano wa Mikabala Unaopima Stadi Moja na Stadi Mchanganyiko.....	36
4.3 Mikabala Unaotumika Zaidi Katika Utungaji wa Maswali ya Mitihani.....	38
4.3.1 Uchambuzi wa Mitihani ya Kiwango Cha Kati ya Mwaka 2017.....	39
4.3.2 Uchambuzi wa Mitihani ya Kiwango Cha Kati ya Mwaka 2018.....	48
4.3.3 Uchambuzi wa Mitihani ya Kiwango Cha Kati ya Mwaka 2019.....	54
4.4 Uchambuzi wa Mitihani wa Ana kwa Ana wa Tarehe 30/07/2018.....	60

4.5 Mtazamo wa Walimu Kuhusu Mkabala Wanaoutumia Zaidi.....	63
4.6 Hitimisho.....	66
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>67</b>
<b>MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>67</b>
5.1 Utangulizi.....	67
5.2 Muhutasari wa Tasnifu.....	67
5.3 Hitimisho.....	68
5.4 Mapendekezo .....	68
5.4.1 Mapendekezo ya Ujumla.....	69
5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Fuatizi.....	69
MAREJEO .....	71
KIAMBATISHO 1: DODOSO LA UTAFITI.....	74
KIAMBATISHO 2: MTIHANI WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 29/09/2017 .....	76
KIAMBATISHO 3: MTIHANI WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 13/12/2017 .....	80
KIAMBATISHO 4: MTIHANI WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 24/08/2018 .....	87
KIAMBATISHO 5: MTIHANI WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 06/09/2018.....	91

KIAMBATISHO 6: MTIHANI WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 31/01/2019.....	95
KIAMBATISHO 7: MTIHANI WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 20/09/2019.....	100
KIAMBATISHO 8: JADWELI LA ORODHA HAKIKI.....	106
KIAMBATISHO NA 9: MTIHANI WA ANA KWA ANA WA KIWANGO CHA KATI WA TAREHE 30/07/2018 .....	107
KIAMBATISHO 10: FOMU YA RIDHAA.....	108
KIAMBATISHO 11: RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI .....	109
KIAMBATANISHO 12: RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI .....	110

## **ORODHA YA MAJADWELI**

Jadweli 3.1 Wasifu wa sampuli ya watoa taarifa za utafiti huu .....	24
Jadweli 4.1 Ufahamu wa Walimu Juu ya Mikabala ya Utungaji Maswali ya Mitihani .	32
Jadweli 4.2 Makabala Unaotumika Zaidi Katika Utungaji wa Maswali ya Mtihani .....	38
Jadweli 4.3 Mtazamo wa Walimu Kuhusu Mkabala Wanaoutumia Zaidi.....	64



## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi**

Sehemu hii itazungumzia kuhusu usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na hitimisho la Sura hii.

#### **1.2 Usuli wa Utafiti**

Upimaji ni jambo la msingi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wanapokuwa katika mazingira ya kimasomo ya kila siku. Pia, ni kitu kinachositahiki kupewa uzito na kipaumbele cha kipekee. Hossam (2015) anaeleza kwamba kuna umuhimu wa upimaji kwa sababu wanafunzi husoma kwa bidii wakiwa vyuoni ili kupata matokeo mazuri, wenye matokeo mazuri hujenga tamaa ya kupata kazi nzuri. Vile vile, upimaji unaweza kutumika kwa ajili ya kufahamu taaluma ya wanafunzi. Kwa mujibu wa Carroll (1961) upimaji hutumika kwa ajili ya kukusanya taarifa kuhusu kiwango cha taaluma ya mtahiniwa. Kiwango ambacho kinakuwa msaada kwa mpimaji ili kuweza kufanya maamuzi ya kimasomo pamoja na kujuwa vipi aendelee na ufundishaji wake. Kwa maneno mengine mitihani hutumika ili kuweza kufahamu kiwango cha elimu alichonacho mtahiniwa kwa sasa na kipi kiboreshwe. Magno (2010) anaeleza kwamba kupatikana kwa viwango vya ufaulu ni moja kati ya njia za kutoa mrejesho kwa wanafunzi na kufahamu mtazamo walionao pamoja na namna walivyoshajihika juu ya somo linalohusika. Lundahl (2014) anafafanua kwa kusema kwamba, viwango vya ufaulu husaidia kuonesha kwa kiasi gani mitihaniilikuwa

na ubora. Wakati wa utungaji wa mitihani lazima mtungaji ayahusishe maswali ya mitihani yake na aina moja wapo ya mkabala wa utungaji wa mitihani. Kwa mujibu wa Oller (1973) kuna mikabala ya upimaji ya aina mbili ambayo huzingatiwa wakati wa utungaji wa maswali ya mitihani. Mikabala hiyo ni mkabala unaopima stadi maalum na mkabala unaopima stadi mchanganyiko kwa wakati mmoja. Kwa kadri ya ufahamu wa mtafiti hadi muda huu bado hajaonautafiti uliofanywa juu ya kuchunguza mkabala unaotumika katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kwa hivyo utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Mkabala wa upimaji ni miongoni mwa mambo muhimu sana katika utungaji wa mitihani, hasa mitihani ya lugha ya pili au lugha ya kigeni. Kwani mkabalawa mitihani ndio unaonesha aina ya mfumo au utaratibu anaotumia mtungaji wa maswali ya mitihani wakati anapotunga mitihani ya somo linalo husika. Licha ya kuwepo umuhimu huo wa uzingatiaji mkabala wa upimaji wakati wa utungaji wa mitihani. Hadi sasa hivi mtafiti wa utafiti huu kwa kadri ya ufahamu wake bado hajaona utafiti uliochunguza mkabala unaotumika katika utungaji wa maswali ya mitihani ya kozi ya Kiswahili kwa wageni, pamoja na kukosekana kwa ushahidi sahihi wa stadi ipi ya lugha inayokusudiwa kupimwa katika maswali ya mitihani ya kozi ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kwa hivyo utafiti huu unalengo la kuchunguza mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa

maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Katika kipengele hiki mtafiti atazungumzia lengo kuu la utafiti na malengo mahsusi kama ifuatavyo: -

##### **1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

##### **1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti**

Malengo mahsusi ya utafiti huu ni: -

- a) Kufafanua kwa kiasi gani walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar wanavyoifahamu mikabala ya utungaji mitihani.
- b) Kubainisha aina ya mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu. Cha Taifa Cha Zanzibar.
- c) Kufafanua mtazamo wa walimu juu ya mkabala wanaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

### **1.5 Maswali ya Utafiti**

Maswali ya utafiti huu ni haya yafuatayo: -

- a) Ni kwa kiasi gani walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar wanavyoifahamu mikabala ya utungaji mitihani?
- b) Mkabala upi unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar?
- c) Walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar wanamtazamo gani juu ya mkabala wanaotumika zaidi katika utungaji wa mitihani hiyo?

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Kuna tafiti mbali mbali ambazo zilifanywa kuhusu maswali ya mitihani yanatungwa na kuulizwa katika mazigira ya kujifunza lugha ya kigeni. Lakini bado kulikuwa na haja ya kufanywa utafiti huu. Utafiti ambao ulichunguza mkabala unaotumika katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Kupitia utafiti huu kunafaida mbali mbali ambazo zilipatikana, faida hizo ni hizizifuatavyo: -

- a) Utafiti huu utachangia kwa kiasi kikubwa maarifa mapya katika taaluma ya utungaji wa maswali ya mitihani ya lugha ya kigeni.

- b) Pia, watafiti wachanga watautumia utafiti huu kwa ajili ya kazi nyingine za kiutafiti zitakazozungumzia mikabala ya utungaji maswali katika mitihani ya lugha za kigeni.

### **1.7 Mawanda ya Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza mkabala unaotumika katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni katika darasa la kiwango cha kati. Kwa kuangalia ufahamu wa walimu juu mikabala ya utungaji mitihani, mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa mitihani na mtazamo wa walimu juu ya mkabala wanaotumia zaidi katika utungaji wa mitihani hiyo.

Wakati wa mchakato wa utafiti huu mitihani ya mwisho ya kiwango cha kati ya mwaka 2017, 2018 na 2019. Pamoja na mitihani wa ana kwa ana wa kiwango hicho uliofanywa mwaka 2018 katika darasa la Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar yalifanyiwa uchambuzi kwa kuzingatia stadikuu nne za lugha. Stadi zenyewe ni stadi ya kusoma, stadi yakuandika, stadi ya kuzungumza na stadi ya kusikiliza.

Mtafiti wa utafiti huu aliifanyia uchambuzi mitihani miwiliya kuandika kwa kila mwaka, kwa kuzingatia maswali mawili (swali la kwanza la ufahamu na swali la mwisho la utungaji) kwa kila mitihani. Wakati wa uchambuzi wa mitihani hiyo mtafiti alizingatia maswali hayo tu, kwani ndio yaliyokuwa na mnasaba na stadiza lugha alizokuwa anazifanyia kazi.

## **1.8 Hitimisho**

Katika sura hii vipengele vilivyofafanuliwa ni utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii imehusika na vipengele viwili muhimu. Kipengele cha kwanza kilikuwa kinahusu kazi mbali mbali zilizotangulia kulingana na utafiti huu. Kazi hizo kwa kiasi kikubwa zilisaidiakubaini mikabala inayotumika katika utungaji wa mitihani ya lugha ya kigeni kama vile Kiswahili na kubaini pengo la utafiti huu. Pili sura hii ilielezea Nadharia ya Tabia ya Umoja (Unitary Trait Hypothesis) kama ilivyoasisiwa na Oller (1979) pamoja na misingi ya nadharia hiyo namna ilivyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu, na mwisho kabisa ni sehemu ya hitimisho ya Sura hii.

#### **2.2 Mapitio ya Maandiko**

Kupitia kipengele hiki, mtafiti alifanya mapitio ya kazi tofauti zilizotangulia kuhusu ufahamu wa walimu juu ya mikabala ya utungaji mitihani, mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya lugha ya kigeni, pamoja na mtazamo walionaawalimu kuhusu mkabala wanaotumia zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya lugha ya kigeni kama vile Kiswahili. Kazi hizo zilifanuliwa kama ifuatavyo:

##### **2.2.1 Ufahamu wa Walimu Juu ya Mikabala ya Mitihani**

Kwa mujibu wa Giraldo (2018) katika utafiti wake alioufanya nchini Kolombia utafiti ambao ulichunguza taaluma, maarifa pamoja na kanuni ambazo zinahitajika katika

upimaji wa lugha ambapo kanuni hizo zinatafsiriwa kama “Ujuzi wa Upimaji wa Lugha” katika utafiti huo alielezea mambo mawili makuu katika upimaji wa lugha; jambo la kwanza lilikuwa ni kutaka kujua nini maana ya taaluma ya upimaji wa lugha na vipi maana hiyo inatofautiana baina ya wadau wakuu wa upimaji wa lugha (kwa mfano wanafunzi na mwalimu).

Giraldo (2018) katika utafiti wake huo alipitia nyaraka za taaluma ya upimaji kutoka kwa wataalamu wa elimu ya ujumla na wataalamu wa elimu ya lugha. Kutokana na mapitio hayo aliweza kuonesha namna ufahamu wa maana ya taaluma ya upimaji wa lugha ilivyozidi kupanuka. Aidha utafiti wake ulielekea zaidi kwenye taaluma maalumu ya upimaji wa lugha ya kigeni na kutoa mapendekezo ya urodha pana kuhusu taaluma ya upimaji, maarifa, na kanuni za upimaji wa lugha unaofanywa na walimu kwa wanafunzi.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo ili walimu waweze kuongeza ubora, uhalisia na uimara wa upimaji wa lugha, nakuweza kufanya upimaji kwakile walichokifundisha kwawanafunzi. Utafiti uligundua kwamba licha ya uelewa walionao walimu kuhusu mikabala ya upimaji bado ipo haja kwa walimu hao kupatiwa mafunzo ya upimaji wa lugha kabla ya kuanza kufundisha. Vile vile wao wenyewe wanaweza kuongeza taaluma yao kwa kupata mafunzo ya ziada wakati wakiwa kazini kupitia makongamano na aina nyingine ya mafunzo ambayo yatawaongezea ujuzi juu upimaji wa lugha (López and Bernal, 2009) akinukuliwa na Giraldo, 2018). Tofauti na Giraldo utafiti huu alijikita zaidi katika kuchunguza mkabala unaotumika katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hata hivyo utafiti wa Giraldo uliweza kumsaidia mtafiti wa utafiti



huu kwa kuonesha kwamba elimu ya upimaji wa lugha ya pili/kigeni kwa ujumla wake ikiwemo mikabala ya upimaji ni kitu muhimu sana. Jambo ambalo walimu wanaofundisha lugha ya pili wanatakiwa waipate kabla ya kuanza kazi ya ufundishaji na wakati wakiwakazini.

Bachman (2010) katika utafiti wake alioufanya katika chuo kikuu cha Kalfonia nchini Marekani. Utafiti ambao ulizungumzia upimaji wa lugha ya kigeni kwa kuwafanyia uchunguzi washika dau tofauti wa elimu juu ya ufahamu wa taaluma ya upimaji wa lugha ya kigeni. Katika utafiti huo alisema kwamba wapimaji wa lugha ya kigeni wanamuunganyiko mmoja wa taaluma pamoja na ukuwaji wa maarifa ya ufahamu wa mambo yenye kuonesha utoaji tafsiri wa muendelezo wa matumizi ya upimaji. Maelezo haya yakiwa na maana ya kwamba walimu pamoja na wadau wengine wa elimu wanao uelewa juu taaluma ya mikabala ya upimaji mitihani ya lugha ya kigeni.

Kwa maelezo haya, utafiti wa Bachman umefanana na utafiti huu katika kuzungumzia uelewa wa taaluma ya upimaji ikiwemo elimu ya mikabala ya utungaji walionayo walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya lugha ya pili. Inapozungumziwa elimu ya upimaji wa lugha ya kigenilazima elimu hiyo ijumuishe maarifa ya mikabala ya ufundishaji na upimaji katika darasa la lugha ya pili/ lugha ya kigeni (Bachman, 2010).

Tran (2012)kupitia utafiti wake ujuwilikanao kwa jina la upimaji wa lugha ya kigeni kwa walimu katika madarasa ya lugha. Kazi ambayo aliifanya katika Chuo Kikuu Cha Teknolojia ya Sayansi huko nchini Marekani, kupitia kazi hiyo yalijadiliwa baadhi ya mambo ya msingi katika upimaji wa lugha ya kigeni yanayohitajika kuwasilishwa

darasani kwa ajili ya kuongeza ujuzi wa utungaji wa mitihani. Kazi hii ilianza na historia ya upimaji, umuhimu wa upimaji na ulazima wa upimaji wa lugha. Tran (2012) katika kazi yake hiyo pia alijadili kuhusu kuwepo mkabala wenye kukubalika katika upimaji wa lugha ya kigeni. Mkabala ambao utauweka mtihani katika hali yenye ubora zaidi kwa kuweza kupata matokeo ya lugha ya pili/kigeni yalio mazuri, pia ni wenye kupunguza wasi wasi na hofu kwa wafanyaji mitihani.

Tran (2012) kupitia kazi yake hiyo alifanya uchunguzi wa mihadhara kumi yenye ubora wa hali ya juu yaliyohusu shahada ya uzamili katika ufundishaji wa Kiingereza kwa wazungumzaji wa lugha nyingine katika nchi ya Marekani kwa kupitia njia ya mtandao. Kupitia utafiti huo aligundua kwamba nusu ya wahadhiri hawatowi mafunzo yanayolingana na upimaji wa lugha ya pili au ufanyaji majumwisho. Wakati hili ni jambo muhimu na la msingi kwa walimu wanaopima lugha ya Kigeni. Coombe na wenzake (2007) wanaeleza kwamba kuna umuhimu na ulazima mkubwa kwa walimu wa lugha ya pili kupatiwa mafunzo kuhusu kanuni za msingi na njia za upimaji. Hii ni kwa sababu si walimu wote wanaofundisha lugha ya pili ambao hupata mafunzo rasimini kuhusu upimaji wa lugha ya pili.

Utafiti wa Tran, unafanana na kukubaliana sana na utafiti huu hasa katika kipengele cha upimaji uelewa wa walimu kuhusu kipengelecha mikabala ya upimaji mitihani ya lugha ya kigeni kama vile Kiswahili ambapo utafiti wa Tran umeonesha kwamba uelewa wa walimu kuhusu mikabala ya utungaji ni hafifu. Kupitia utafiti huu uelewa wa walimu kuhusu mikabala umeonekana ni wakuridhisha. Hata hivyo, data za utafiti huu

zilionesha kwamba bado kuna haja kwa walimu wanaopima lugha ya kigenikuongeza elimu ya upimaji, hasa kwenye kipengele cha mikabala ya mitihani.

### **2.2.2 Mkabala Unaotumika Zaidi Katika Utungaji wa Mitihani**

Bachman (2010) katika utafiti wake alioufanya katika Chuo Kikuu Cha Kalfonia Nchini Marekani. Utafiti ambao ulizungumzia taaluma ya upimaji wa lugha ya kigeni, katika utafiti huo aliwanukuu (Lado, 1961 na Carroll, 1961, 1968) kwa kusema kwamba mwanzoni ilielezwa wazikwamba modeli ya uwezo wa lugha ambayo hutumika kwa ajili ya upimaji wa lugha ni mkabala wa ujuzina vipengele. Kupitia utafiti huo kulitolewa ufafanuzi uliowazi baina ya ujuzi na uwezo kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kukawa na maelezo kuhusu mkabala, njia au aina ya upimaji. Stadi za lugha zilizohusika kupitia mkabala wa ujuzi na vipengele ni stadi ya kusikiliza, stadi ya kuzungumza, stadi ya kusoma na stadi kuandika, wakati vipengele vilivyomo ni alama na vituo, sarufi, msamiati na kipengele cha maana za kiutamaduni.

Wananadharia wa kisasa, wajifunzaji na wafundishaji wa lugha wanauelezeamkabala wa ujuzi na vipengele kwa uwazi kuwa ni wa kwanza katika historia za upimaji wa lugha. Mkabala wa ujuzi na vipengele umekuwa na ushawishi mkubwa na imeelezwa kuwa mkabala huu ni kizazi cha tathimini chenye kuchukuwa nafasi zaidi kwa lugha ya kigeni au lugha ya pili katika nchi ya Marekani, na kuonesha kwamba wapimaji na waandaaji wa maswali ya mitihani wanauelewa mkubwa juu ya aina hii ya mkabala wa upimaji wa lugha (Bachman, 2010).

Maelezo haya yanaumuhimu mkubwa katika utafiti huu kwani stadi za lugha zilizozingatiwa katika mkabala wa ujuzi na vipengele ni stadikuu nne za lugha juu ya uelewa wa walimu kuhusu mikabala ya utungaji mitihani. Wakati ndio zile zile zilizozingatiwa na mtafiti wa utafiti huu, tofauti iliyokuwape ni kwamba kazi hii haikuzingatia stadi ndogo za lugha ukitoa stadi kuunneza lugha. Kwa hivyo, kwa mujibu wa mtafiti wa utafiti huu, matokeo ya kazi hii yalionesha kwamba mkabala unaotumika zaidi ni mkabala unaopima stadi nyingi za lugha kwa wakati mmoja kama ulivyo utafiti wa Bachman.

Kwa mujibu wa Hancock (2006) kupitia utafiti wake unaoitwa ufundishaji na upimaji wa lugha alioufanya katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Ohio Nchini Kolumbus. Kazi ambayo iliandaliwa kutokana na mmarekani mwenye uzoefu wa kufundishana kufanya upimaji wa lugha za kigeni kwa zaidi ya miaka 25. Kupitia kazi hiyo alitumia maigizo pamoja na mahojiano ikiwa ni njia ya ukusanyaji wa data. Katika kazi hiyo alisisitiza kwamba wafundishaji na wapimaji wa lugha ya kigeni au lugha ya pili lazima waviunganishe vitu viwili kwa wakati mmoja yaani mkabala unaotumika katika ufundishaji na mkabala unaotumika katika upimaji wa lugha ya kigeni lazima uwe mmoja.

Hancock (2006) anaeleza kwamba mkabala wa kuutumia zaidi katika ufundishaji na upimaji wa lugha ya kigeni ni mkabala wa mawasiliano, mfumo huu ulisisitizwa Dunia nzima na kupewa kipaumbele katika ufundishaji na upimaji ufahamu wa lugha ya kigeni, kutokana na hali hii ndio maana inatiliwa mkazo kwa wajifunzaji wa lugha ya kigeni

kupimwa kile ambacho wanaweza kukifanya katika lugha na sio wanachokijua (Hancock, 2006).

Utafiti wa Hancock umesaidia sana kuuboresha utafiti huu kwani mtafiti wa utafiti huu wakati wa ufanyaji kazi yake alizingatia stadikuu nne za lugha huku akiwa anaamini kwamba mjifunzaji wa lugha ya kigeni ili awe na uwezo mzuri wa kuitumia lugha nayojifunza katika mawasiliano lazima ahitimu vizuri stadi zote kuu za lugha.

Kwa mujibu wa Moeller na Catalano (2015) kupitia kazi yao inayoitwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigenikazi ambayo waliifanya katika Chuo Kikuu Cha Lincoln Nchini Marekani. Kupitia kazi hiyo walisemakwamba mkabala unaositahiki kutumiwa zaidi kwa ajili ya upimaji katika darasa la lugha ya kigeni ni mkabala wa kimawasiliano. Kupitia mkabala huu, imeelezwa kwamba wataalamu wa lugha ya kigeni pamoja na walimu wanaofundisha lugha ya kigeni jukumu lao nikuongeza hamu ya kushiriki katika upimwaji kwa wajifunzaji, kurahisisha upimaji, kuwafanya wanafunzia kuwa na hamasa zaidi ya kujifunza na kuwapunguzia wanafunzi hali ya kuchanganyikiwa wakati wa ufanyaji mtihani(Moeller na Catalano, 2015).

Katika kuonesha umuhimu wa mkabala wa mawasiliano kazi ya Moeller na Catalano ya mwaka 2015 ililingana sana na kazi ya Hancock ya mwaka 2006.Kupitia kazi hizombili, kiukweli kazi hii ilipata faida sana ya kuongeza ubora wake kwani moja ya stadi za lugha ilizozifanyia kazi ni stadi ya mazungumzo, ingawa kuna tofauti kubwa na majibu ya utafiti huu, hii ni kwa sababu wakati mtafiti alipowataka watoa taarifa wake waorodheshe aina za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha hawakutaja mkabala wa

mawasiliano. Hata hivyo, stadi ya mazungumzo ni moja kati ya stadi za lugha zilizozingatiwa katika kazi hii.

Sambamba na hayo, bado kuna umuhimu mkubwa kwa wajifunzaji wa lugha ya kigeni kuweza kupata ujuzi na uzowefu wakuitumia lugha kwa mujibu wa mazingira na mahitaji yao.

Kwa mujibu wa Alhussain (2009) kupitia kazi yake ijuwilikanayo kwa jina la mapendekezo juu ya utumiaji wa mkabala mjumuishi ili kuboresha ujuzi wa mawasiliano kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya kigeni. Utafiti huo aliufanya katika Chuo Cha Kimataifa Cha Sayansi ya Afya kilichopo Riyadh, Saudi Arabia. Wanafunzi 105 wa kike walifanyiwa mtihani wa mazungumzo ya mdomo uliozingatia mkabala mjumuishi (mkabala unaopima stadi nyingi za lugha kwa wakati mmoja) katika njia ya ulinganishaji baina ya wanafunzi waliosomeshwa stadi ya sarufi, stadi ya kusikiliza, stadi ya kusoma na stadi ya kuzungumza kwa njia ya mjumuishi na wale waliosomeshwa stadi hizo kwa njia ya kutenganishwa (Alhussain, 2009).

Majibu ya utafiti huo yalionesha kwamba wanafunzi waliosomeshwa na kupimwa kwa kutumia mkabala mjumuishi ikiwa ni ujifunzaji wa Kiingereza kama lugha ya kigeni walifanikiwa zaidi juu kupata ujuzi wa mawasiliano, na kuthibiti kwamba ufundishaji na upima kwa kupitia mkabala mjumuishi kwa wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya kigeni ni jambao lilibora zaidi. Kutokana na matokeo hayo utafiti wa Alhussain ulikuwa na mchango mkubwa katika kuonesha uaminikaji wa taarifa za utafiti huu, kwani majibu ya utafiti huu yalionesha kwamba upimaji wa lugha ya kigeni kwa

njia mjumishi ndio unaokubalika zaidi katika upimaji ingawa utafiti huu ulichunguza kipengele cha upimaji peke yake na haukukifanyia kazi kipengele cha ufundishaji.

### **2.2.3Mtazamo wa Walimu Kuhusu Mkabala Unaotumika Zaidikatika Upimaji**

Kwa mujibu wa Bachman (2010)mkabala wa ujuzi na vipengele una nafasi kubwa katika upimaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni kwani katika upimaji wake unazingatia stadikuunneza lugha. Kuipima lugha ya kigeni kwa kuzingatia stadi kuu ni jambomuhimu sana. Kwani mjifunzajiwa lugha ya kigeni ili awe na umahiri mzuri katika kuitumia lugha inayohusika ni vizuri apimwe kwa kuzingatia stadi kuu soteili uonekane uwezo wake wa kuitumia lugha hiyo kwa ujumla(Hughes, 1989).

Utafiti wa Bachman (2010) unakwenda sambamba na utafiti huu kwa sababu mtafiti wa utafiti huu alizingatia stadi kuu nne za lugha kama alivyofanya Bachaman, hasa katika kulitafutia majibu lengo la pili la utafiti huu.Matokeo ya utafiti huu yalizidi kuboreka iliposemwa kwamba uzingatiaji wa stadikuunne za lugha ni kitu cha msingi sana katika ufundishaji na upimaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni (Bachman, 2010).

Aidha, kwa mujibu wa Hancock (2006) kupitia kazi yake hiyo aliyoifanya katikaChuo Kikuucha Taifa Cha Ohlo Nchini Kolumbus, alisema kwamba wajifunzaji kuweza kuitumia lugha kwa mujibu wa mahitaji yao ndicho kitu ambacho kinapelekea mkabala wa mawasiliano kutumika na kuwa maarufu. Kwa sababu wanafunzi huhitaji kuzungumza kwa kutumia simu, au huhitaji kusoma na kuandika barua pepe kwa watu wao wa karibu. Pia, huweza kusoma, kuandika, kuzungumza na kuweza kusikia lugha wanayojifunza(Hancock, 2006).

Hali hii ya wajifunzaji kuweza kuitumia lugha kwa mujibu wa mahitaji yao ndio sababu iliyopelekea mkabala huu kukubalika na kupewa kipaumbele kwani umesaidia sana kuweza kufikia lengo la kujifunza lugha ya pili au lugha ya kigeni. Maelezo haya yamekubaliana sana na matokeo ya utafiti huu, kwa sababu lengo la kujifunza lugha ya kigeni ni kupata maarifa ya kuweza kuitumia lugha husika katika mazingira ya kawaida jambo ambalo linahitaji kuwa na ujuzi wa stadi kuu nne za lugha.

Kwa upande wa Moeller na Catalano (2015) kupitia kazi yaoinayoitwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni, kazi ambayo waliifanya nchini Marekani, kupitia kazi hiyo mkabala wa kimawasiliano waliupa nafasi zaidi katika mchakato wa upimaji wa wanafunzi. Kwa sababu kupitia mkabala huomajukumu ya mwalimu yalirahisika na kuwafanya wajifunzaji kuwa na uwezo wa kutoa maana ya maneno, kuchanganjika na jamii na kutengeneza maswali ambayo yataweza kuwafanya washauriane katika kupata maana ya lugha ambayo itaendana na mazingira ya kijamii. Pamoja na hayo, maswali yatakayoandaliwa na walimu yatazingatia kwa kiasi gani umahiri wa lugha unaweza kufikiwa(Moeller na Catalano, 2015).

Mtazamo huu ulikwenda sambamba na kazi hii kwani maswali ya mitihani yaliyozingatiwa katika uchambuzi wa nyaraka pamoja na nadharia iliyotumika katika utafiti huu, vyote kwa pamoja vilizingatia uwezo wa kuitumia lugha katika mazingira ya kawaida ya kijamii pamoja na kuona umuhimu wa kuipima lugha yote kwa ujumla wake.



Kwa upande wa Alhussain (2009) kupitia utafiti wake alioufanya katika Chuo cha Kimataifa cha Sayansi ya Afya kilichopo Riyadh, Saudi Arabia, kwa wanafunzi 105 waliokuwa wanajifunza ukunga, wanafunzi hao walifanyiwa mtihani wa mazungumzo. Matoke ya utafiti huo yalionesha kwamba mkabala mjumuishi katika ufundishaji na upimaji ndio wenye kufaa zaidi kwa wajifunzaji wa lugha ya pili/kigeni kuliko njia ya zamani ya kuifundisha na kuipima lugha ya kigeni kwa njia ya kuzitenganisha stadi za lugha. Kwa sababu mkabala mjumuishi humsaidia mjifunzaji wa lugha ya kigeni kupata muda mkubwa wa kufanya mazungumzo na kuweza kuitumia lugha katika mazingira yake ya kawaida nje ya mazingira ya kujifunza baada ya kuzihitimu stadi za lugha kwa ujumla wake (Alhussain, 2009).

Majibu ya utafiti wa Alhussain yalisaidia kuyafanya matokeo ya utafiti huu kuwa ni yenye kuaminika kwa kuonesha umuhimu wa matumizi ya mkabala mjumuishi katika upimaji wa wanafunzi wanaojifunza lugha ya kigeni ingawa utafiti huu haukuchunguza matumizi ya mkabala mjumuishi katika ufundishaji wa lugha ya kigeni.

### **2.3 Pengo la Utafiti**

Katika mchakato mzima wa kutunga mitihani ya kozi yeyote ile kuna mambo mengi ambayo huwa na ulazima wa kuhusishwa, miongoni mwa mambo hayo ni kama vile mkabala utakaotumika katika utungaji wa mitihani inayohusika. Miongoni mwa kozi zinazosomeshwa katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar, ni kozi ya ufundishaji Kiswahili kama lugha ya kigeni ambapo wanafunzi wanaosoma kozi hii na wao huandaliwa mitihani kwa kuzingatia mkabala fulani kama zilivyo kozi nyingine.

Hadi muda huu kwa kadri ya ufahamu wa mtafiti bado hajaona tafiti zilizochunguza mkabala unaotumika wakati wa utungaji maswali ya mitihani ya kozi ya lugha ya kigeni. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

#### **2.4 Kiunzi Cha Nadharia**

Nadharia iliyotumika katika ukamilishaji wa utafiti huu, ilikuwa Nadharia ya Tabia ya Umoja (Unitary Trait Hypothesis) nadharia ambayo ili asisiwa na Oller (1979).

Kwa mujibu wa Oller (1979) msingi mkuu wa nadharia ya tabia ya umoja ni kuipima lugha ya kigeni katika hali ya mjumuishi. Kuna umuhimu mkubwa wa kuitumia nadharia hii katika upimaji wa lugha ya kigeni, hii ni kwa sababu ili mtu awe mmahiri mzuri wa lugha ya kigeni lazima awe na uwezo mkubwa kuzitumia stadi kuuzote za lugha inayohusika.

Oller (1979) kupitia nadharia hii alieleza kwamba umahiri wa lugha ni kitu kinachopimwa katika muunganyiko zaidi, kuliko kupimwa katika hali ya kutenganishwa. Kwa hivyo, msamiati, sarufi, fonolojia, stadi kuu nne za lugha, pamoja na vipengele vya lugha si vizurikwa kila kimoja kupimwa peke yake.

Kwa mujibu wa Oller (1979) msingi mwengine wa nadharia ya tabia ya umoja unaeleza kwamba, lugha lazima ipimwe kwa mujibu wa mazingira halisi ya watumiaji wa lugha hiyo, hii ni kwa sababu kiasili lugha inajuwilikana vizuri kuwa ni mfano wa mjengeko

mgumu wa vipengele vilivyomo katika muendelezo wa kimadaraja, madaraja ambayo yamekuwepo kutokana na vipengele tofauti vya lugha.

Taaluma ya sarufi tarajiwa imeonesha ukweli kwamba muunganyiko wa vipengele na madaraja yaliyomo katika lugha, vinapatika kwa watumiaji wa lugha katika mazingira yao halisi ya kimaisha. Hii ni kwa sababu mazingira halisi ya watumiaji wa lugha yameungana na mazingira fulani ya kilughawiya (Oller, 1986).

Kwa mujibu wa Bachman (1995) shauku ya wapimaji wa lugha katika utungaji wa mitihani ya lugha yenye ubora, iliibuliwa upya katika miaka ya 1970 kupitia nadharia ya tabia ya umoja iliyoasisiwa na Oller.

Oller (1979) aliyabua mambo ya ujumla ambayo yalitafsiriwa kuwa ni tabia ya umoja “umahiri wa lugha wa ujumla”. Bachman (1995) sio tu, nadharia hiyo ilizihamasishatafiti za Oller, pia ilianzisha mjengeko wa ubora kuwa ni jambo la msingi la kuzingatia katika utafiti unaopima lugha ya kigeni, na kuendeleza hamasa mpya katika uchambuzi wa mambo na kuwahatua ya kiufundi katika kuandaa mitihani ya lugha yanayoendana na mazingira yanayohusika.

Aidha, Mtafiti wa utafiti huu alitumia Nadharia ya Tabia ya Umoja (Unitary Trait Hypothesis) katika kuchambua lengo la kwanza la utafiti huu juu ya swala zima la kuangalia ufahamu wa walimu kuhusu mikaba ya utungaji wa mitihani ya lugha ya kigeni kwa kuzingatia mihimili ya nadharia hii ambapo ilizungumzia mikabala ya

upimaji kwa sababu ni jambo la msingi kuwa na ujuzi nalo kwa mwalimu anayetunga mitihani ya lugha ya kigeni.

Sambamba na hayo, mtafiti alitumia Nadharia ya Tabia ya Umoja kama muongozo wakati wa zoezi zima la uchambuzi wa mitihani ya mwisho ya kiwango cha kati katika darasa la Kiswahili kwa wageni kwa ajili ya kupata majibu ya lengo la pili la utafiti huu. Uchambuzi huo ulifanywa kwa kuzingatia maswali yaliyobeba stadi kuu nne za lugha pamoja na matumizi ya lugha kwa mujibu wa mazingira ya mtumiaji ambayo ndio misingi mikuu ya nadharia ya tabia ya umoja.

Vile vile, mtafiti wa utafiti huu alitumia nadharia ya Tabia ya Umoja wakati wa uwasilishaji na uchambuzi wa data za lengo la tatu ambalo lilikuwa linataka kujua mtazamo wa walimu juu ya mkabala wanaoutumia zaidi. Umuhimu wa nadharia hii ulionekana katika lengo hili kutokana na msisitizo wake wa kuipima lughaya kigeni kwa mujibu wa malengo ya wajifunzaji kama vile lengo la tatu la utafiti huu lilivyotaka kujua mtazamo wa walimu juu ya mkabala wanaoutumia zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni.

## **2.5 Hitimisho**

Sura hii ilianza na utangulizi pamoja na kuangalia kazi mbali mbali zilizotangulia, kazi ambazo zilihusiana na utafiti huu. Vile vile Sura hii ilieleza kuhusu pengo la utafiti pamoja na nadharia ambayo ilitumika katika utafiti mzima.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inashughulika na mbinu mbali mbali ambazo zilitumika katika mchakato mzima wa ufanyaji utafiti huu. Sura hii imegawika katika sehemu kuu tisa. Sehemu ya kwanza inajadili kuhusu mkabala wa utafitina aina zake. Sehemu ya pili ya utafiti huu inajadilikuhusu eneo la utafiti, sehemu ya tatu inajadili kuhusu watoa taarifa, sampuli na usampulishaji. Sehemu ya nne inajadili mbinu mbali mbali zilizotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Sehemu ya tano inahusika na zana za utafiti. Sehemu ya sita njia ya uchambuzi wa data za utafiti. Sehemu ya saba inahusu maadili ya utafiti. Sehemu ya nane inahusu uaminikaji wa data na sehemu ya tisa itakuwa hitimisho la Sura hii.

#### **3.2 Mkabala wa Utafiti**

Utafiti huu alitumia mkabala mseto, kwani ndio mkabala unaopendekezwa na wataalamu wengi wa kileo katika ufanyaji wa utafiti(Das, 1983).Sehemu ndogo ya utafiti huu ilitumia mkabala wa takwimu. Uchambuzi wa data kwa njia ya takwimu ulitumika kwa ajili ya data za swali la kwanza. Utafiti huu ulitumia njia hii kwa sababu ulihitaji kupata majibu ya kiasilimia pamojana kujua kiwango cha ufahamu kwa walimu juu mikabala ya utungajimitihani ya lugha(Punch na Punch, 2005). Mtafiti alizipanga data kutokana na maudhui yake na kuziweka katika makundi yaliyofanana, pamoja na

kuzitolea ufafanuzi ili kuweza kupata majibu ya maswali yaliyohusika na utafiti wake(Pacitti, 1998).

Sehemu kubwa ya utafiti huu ilitumia mkabala wa maelezo hasa katika uchambuzi wa data zililizotumika kwa ajili ya kujibuswali la pili na swali la tatu. Wakati wa uchambuzi wa data zilizojibu maswali hayo mawili mtafiti alitumia njia ya maelezo kwasababu alitaka kujua mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali kwa kuzingatia uzoefu, mawazopamoja na mtazomo walionao walimujuu ya mkabala huo. (Holland na Rees, 2010).

Kabla ya kuzichambua data hizo, mtafiti alizipitia ili kupata data ambazoziliendana na mahitaji ya maswali yake. Baada ya mtafiti kuzipitia data hizo aliziweka bayana na mwisho alizifanyia majumuisho ya majibu yake, pamoja na kufanya uthibitisho kwa mujibu wa maswali yaliyohusika na data hizo (Miles na Huberman, 1994).

### **3.3 Eneo la Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Mjini Unguja katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar kupitia Kampasi yake iliyopo Vuga. Katika Idara ya Kiswahili kwa Wageni ya chuo hicho. Idara ya Kiswahili kwa Wageni ndio iliyotumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Kwa sababu ndio hasa yenye mnasaba na utafiti huu. Idara hiyo, inajukumu la kusomesha Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine, inamamlaka ya utungaji mitihani ambayo huwa wanafanya wanafunzi wa kigeni wanaojifunza Kiswahili chuoni hapo.

Pia, idara hiyo inawalimu wanaosomesha Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine. Huku ikizingatiwa kwamba mitihani ya kiwango cha kati inayotungwa idarani hapo ndio yaliyohitajika kwa ajili ya kupata data zilizotumika kwa lengo la kujibu swali la pili, na walimu waliotunga mitihani hiyo walihitajika kwa ajili ya kujaza dodoso lilosaidia kupata data zilizojibu swali la kwanza hadiswali la tatu la utafiti huu.

Sababu hizo ndizo zilizompelekea mtafiti wa utafiti huu kuichagua Idara ya Kiswahili kwa Wageni iliopo Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar katika kukamilisha kazi yake hii. Kwani mtafiti anaweza kuchagua eneo la utafiti ambalo litakuwa na unafuukwake kwa mujibu wa kazi aliyoikusudiakuifanya (Stake, 2006).

### **3.4 Watoa Taarifa, Sampuli na Usampulishaji**

#### **3.4.1 Watoa Taarifa**

Watoa taarifa katika utafiti huu, walikuwa walimu wanaosomesha kozi ya Kiswahili kama lugha ya kigeni katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Kwani hao ndio waliokuwa na uwezo mkubwa wa kuupatia utafiti huu data zilizohitajika kwa mujibu wa malengo ya kazi hii.

#### **3.4.2 Sampuli**

Utafiti huu ulihusisha watoa taarifa, watoa taarifa watatu walikuwa wanaume na watoa taarifa wanne walikuwa wanawake. Watoa taarifa hao waliteuliwa kutoka katika kundi la walimu tisa wanaosomesha pamoja na kutunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaosoma kozi ya Kiswahili kama lugha ya kigeni kutokana na uwezekano wa kupatikana kwao ili waweze kushiriki katika utafiti huu. Walimu hao

wakiwa ni wenye kutofautina kwa vipengele tofauti kama wanavyoonekana katika ufafanuzi wa jadweli lifuatalo hapo chini: -

### Jadweli 3.1

#### *Wasifu wa sampuli ya watoa taarifa za utafiti huu*

NA	JINA LA MWALIMU	JINSI	UZOEFU WA KAZI	ELIMU	FANI
1	A	Mke	Miaka 5	Uzamili	Kiswahili
2	B	Mke	Miaka 20	Uzamili	Kiswahili
3	C	Mke	Miaka 10	Uzamili	Kiswahili kwa wageni
4	D	Mke	Miaka 8	Uzamili	Kiswahili kwa wageni
5	E	Mme	Miaka 5	Uzamili	Kiswahili
6	F	Mme	Miaka 26	Shahada	Ualimu
7	G	Mme	Miaka 22	Uzamili	Kiswahili

**Chanzo:** Uwandani (Agosti: 2020).

**Tambihi:** Majina yaliyotumika katika jadweli hili sio majina halisi ya watoa taarifa za utafiti huu.

#### 3.4.3 Usampulishaji

Wakati wa ukusanyaji data za utafiti huukupitia njia ya dodoso mtafiti alitumia usampulishaji tajwa. Data zilizotumika kwa ajili ya kujibu swali la kwanza zilichambuliwa kwanjia ya takwimu, pamoja na data zilizotumika kwa ajili ya kujibu swali la tatu, na data ambazo zilitoa majibu ya lengo la pili zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Kigezo kilichotumika ni kumpata mwalimu mwenye uzoefu wa miaka mingi katika usomeshaji na utungaji mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Mtafitiwa aliyepewa dodoso kwa mara ya kwanza ndie alietowa maelekezo ya kumpata mtoa taarifa mwingine mwenye vigezo na sifa kama zake huku kukizingatiwa na



upatikanaji wake. Aina hii ya usampulishaji ilimshawishi mtafiti kuweza kuitumiakatika utafiti huu kwa sababu ndio yenye uwezo wa kuwapata watoa taarifa sahihi kwa mujibu wa malengo ya utafiti wake.

### **3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data**

Mbinu hizi hutumika ili kukusanyia data kwa lengo la kupata taarifa za kiutafiti ambazo hutumiwa ili kutoa majumwisho ya kazi nzima ya utafiti husika (Trompo na Kombo, 2005). Kupitia utafiti huu mtafiti alitumia mbinu mbili ikiwa ni njia za ukusanyaji majibu kutoka kwa watoa taarifa kama ifuatavyo: -

#### **3.5.1 Mbinu ya Dodoso**

Utafiti huu ulitumia mbinu ya dodoso kwa ajili ya kukusanya data zilizojibu swali la kwanza hadi swali la tatu la utafiti huu. Kwa mujibu wa Roopa na Rani (2012) njia hii hutumika ili kutoa nafasi ya kudhibiti siri kwa watoa taarifa na kuwapa faragha ya kutoa mawazo na maoni yao dhidi ya maswali ya dodoso yanayohusika. Mtafiti aliichagua njia hii kuwa ni moja katika njia za ukusanyaji wa taarifa kwani husaidia kutoa taarifa zenye usahihi, hupunguza upendeleo, hutumia gharama ndogo na haihitaji muda mkubwa hata kama kwa idadi kubwa ya watafitiwa (Cohen, 2009). Taarifazilizojibu swali la kwanza zilichambuliwa kwa njia ya takwimu na taarifa zilizojibu swali la pili na la tatu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo(Roopa na Rani 2012).

### **3.5.2 Mbinu ya Uchambuzi wa Nyaraka**

Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchambuzi wa nyaraka kwa ajili ya kupata majibu ya swali la pili la utafiti huu. Uchambuzi wa kina ulifanywa kwa mitihani ya Kiswahili kwa wageni iliyotumika katika upimaji wa wanafunzi wa kozi hiyo katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Mitihani hiyo ilikuwa ni yale ya kumaliza kozi kwa wanafunzi wa kiwango cha kati (mitihani ya mwisho), kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo yaani mwaka 2017, 2018 na 2019, pamoja na mitihani wa ana kwa ana wa mwaka 2018.

Kwa kila mwaka mtafiti aliifanyia uchambuzi mitihani miwili, kwa kuzingatia maswali mawili kwa kila mitihani, swali la kwanza lililokuwa linahusiana na usomaji wa habari, ambapo baada ya kwisha kuisoma habari mwanafunzi alitakiwa kuyajibu maswali yaliyotokana na habari hiyo, na swali la mwisho lililokuwa linahusiana na utungaji wa insha, ambapo mwanafunzi alitakiwa kuchagua mada moja katika swali husika na kuitungia insha. Mtafiti aliyazingatia maswali hayo mawili katika mitihani hiyo, kwani maswalihayo ndio haswa yaliyokuwa yanaendana na malengo ya utafiti huu. Vile vile, mtafiti alichagua mitihani hii ya miaka mitatu ya karibuni kwa ajili ya kupata taarifa zinazokwenda na wakati zaidi.

Aidha, lengo la kutumia mbinu hii ilikuwa ni kupata picha halisi ya namna mitihani inavyotungwa na walimu kulingana na mkabala wanaotumia katika utungaji wa maswali ya mitihani hiyo. Cohen (2009) anaelezea kwamba mbinu hii humpa mfanyaji utafiti nafasi ya kukusanya data kutoka katika mazingira halisi ya kijamii, vile vile humuwezesha mtafiti kupata data za moja kwa moja juu kile anachokihitaji. Kwa

upande wa Yin (2003) ushahidi unaotokana na nyaraka ni chanzo muhimu cha ukusanyaji taarifa za utafiti, na chanzo ambacho kinaweza kutumika kwa ajili ya kuongeza ushahidi unaotokana na vyanzo vyengine.

### **3.6 Zana za Ukusanyaji wa Data**

Zana zilizotumika wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti huu ilikuwa orodha hakiki peke yake. Zana hii ilitumika wakati wa uchambuzi wa nyaraka (mitihani) zilizotumika katika utafiti huu.

#### **3.6.1 Orodha Hakiki**

Mtafiti wa utafiti huu alitumia orodha hakiki wakati wa uchambuzi wa mitihani ya mwisho ya darasa la Kiswahili kwa wageni la Kiwango cha kati ya mwaka 2017, 2018 na 2019 pamoja na mtihani wa ana kwa ana wa mwaka 2018. Orodha hakiki ilimuongoza mtafiti wakati alipokuwa anahakiki stadi kuu nne za lugha kama zilivyojitokeza katika mitihani hiyo.

### **3.7 Uchambuzi wa Data**

Katika utafiti huu, data zilizokusanywa zilipitiwa kwa umakini, zilipangwa katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti, zilihakikiwa na kufanyiwa uchambuzi wa kina. Baada ya hapo data za aina moja ziliwekwa pamoja ili kupanga ugawaji wa matokeo. Uchambuzi wa data ulihusiana na malengo mahsusi ya utafiti huu ili kuona ukweli ambao ulipatikana kupitia mbinu ya dodoso na mbinu ya uchambuzi wa nyaraka (mitihani). Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mkabala mseto. Njia ya

takwimu ilitumika kwa ajili ya kuchambua data za swali la kwanza na data zilizokusanywa kwa ajili ya kujibu swali la pili na swali la tatu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo.

### **3.8 Maadili ya Utafiti**

Wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Mtafiti aliwaweka wazi watoa taarifa wake juu ya lengo halisi la utafiti huu pamoja na kuwapatia fomu ya ridhaa kabla ya kuwapa dodoso la utafiti. Mtafiti aliwaomba watoa taarifa walijaze dodoso hilo ili aweze kupata data zitakazomsaidia kujibu swali la kwanza hadi swali la tatu la utafiti huu. Mtafiti alifanya hivyo ili kuwatoa hofu watoa taarifa wake, kwani fomu ya ridhaailionesha wazi kwamba data watakazozitoa zitakuwa siri na zitatumika kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu tu na sivyenginevyo. Pia, watoa taarifa hao walipewa uhuru wa kujitoa katika utafiti wakati wowote ambapo wangeamua kufanya hivyo.

Sambamba na hayo mtafiti wa utafiti huualihakikisha kwamba amekamilisha taratibu zote za kisheria zinazompa ruhusa ya kufanya utafiti, kwa kuanzia chuoni ambapo ndio eneo lake la kukusanyia data za utafiti. Pamoja na kukamilisha masharti kutoka katika mamlaka zote za Serikali zilizohusika na utafiti huu.

### **3.9 Uaminikaji wa Data**

Data za utafiti huu zinaaminika kwa kiwango kikubwa kwani upatikanaji wake ulizingatia njia zenye uwezo mkubwa wa kuweza kukusanya data zinazohusika. Kuna data zilizokusanywa kwa njia ya dodoso. Data ambazo zilitumika kwa ajili ya kujibu swali la kwanza hadi swali la tatu la utafiti huu. Data za swali la kwaza zilichambuliwa

kwa njia ya takwimu, njia ambayo inakubalika zaidi kwa ajili ya kupata majibu yaswali la kwanza la utafiti huu, kwani swali hilo lilitaka kujua kiwango cha ufahamu kwa walimu juu ya mikabala ya utungaji maswali ya mitihani ya kozi ya Kiswahili kwa wageni chuoni hapo(Warren, 2020).

Vile vile data zilizopatikana kwa njia hiyo hiyo ya dodoso kwa ajili ya kujibu swali la pili na swali la tatu na zile zilizopatikana kwa njia ya uchambuzi wa nyaraka kwa ajili ya kujibu swali la pili tu la utafiti huuzilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Kwa sababu mtafiti alitaka kujua uzoefu na mtazamo walionao walimu juu ya mkabala wanaoutumia zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni(Addo na Eboh, 2014).

Usampulishaji tajwa ndio uliotumika kwa ajili ya kupata data zilizokusanywa kwa njia ya dodoso. Baada ya kujazwa madadoso hayoambayo yalikuwa na maswali ya aina moja. Mtafiti aliyapitia kwa umakini na alipokuwa hajafahamu alitafuta ufafanuzi kutoka kwa wajasaji wa madodoso hayo.

Kwa mujibu wa mkabala uliotumika katika utafiti huu, vigezo vilivyotumika katika kuwapata watoa taarifa kwa ajili ya ujazaji wa dodoso, pamoja na maswali ya mitihani yaliyozingatiwa wakati wa uchambuzi wa nyaraka. Vitu vyote hivyo kwa ujumla wake vilisaidia sana kuweza kuzifanya data za utafiti huu kuwa za uhakika na zenye kuaminika.

### **3.10 Hitimisho**

Sura hii ilishughulika na mbinu mbali mbali, mbinu ambazo zilitumika katika mchakato mzima wa ufanyaji utafiti, sura hii iligawika katika sehemu kuu tisa, sehemu ya kwanza ilijadili kuhusu utangulizi wa sura hii. Sehemu ya pili ilijadili mkabala wa utafiti. Sehemu ya tatu ilijadili eneo lililohusika na utafiti huu. Sehemu ya nne ilijadili watoa taarifa, sampuli na usampulishaji. Sehemu ya tano ilijadili mbinu mbali mbali zilizotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa data za utafiti. Sehemu ya sita ilihusiana zana za utafiti, sehemu ya saba ilikuwa uchambuzi wa data. Sehemu ya nane ilizungumzia maadili ya utafiti nasehemu ya tisa ilizungumzia uaminikaji wa data za utafiti huu.

## **SURA YA NNE**

### **UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data ambazo zilipatikana kupitia utafiti huu. Kwa ujumla utafiti huu ulikuwa na maswali matatu, maswali ambayo yalihitaji kupatiwa majibu kwa ajili ya kukamilisha malengo ya kazi husika. Kwa hivyo, uwasilishaji na uchambuzi wa data hizo, vimefanyika kwa kuzingatia maswali matatu ya msingi ya utafiti huu, baada ya uwasilishaji na uchambuzi wa data, sura hii itamaliziwa kwa hitimisho kama ifuatavyo: -

#### **4.2 Ufahamu wa Walimu Juu ya Mikabala ya Utungaji Maswali ya Mitihani**

Kupitia swali la kwanza la utafiti huu, mtafiti alitaka kujua kwa kiasi gani walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar wanavyoifahamu mikabala ya utungaji maswali ya mitihani. Katika kulitafutia majibu swali hili mtafiti alitumia mbinu ya dodoso ikiwa ni njia ya ukusanyaji wa data. Uchambuzi wa kina kuhusu data zilizokusanywakutoka kwa watoa taarifa kwa ajili kujibu swali la kwanza utaonekana kupitia jadweli lifuatalo: -

### Jadweli 4.1

#### *Ufahamu wa Walimu Juu ya Mikabala ya Utungaji Maswali ya Mitihani*

**Ufunguo:** Me sawa sawa na mwanamume, Ke sawa sawa na Mwanamke, Deg sawa sawa na Shahada ya Kwanza, Mast sawa sawa na Uzamili, PHD sawa sawa na Uzamivu, TEKSOL sawa sawa na Kufundisha Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine, Kisw sawa sawa na Kiswahili na (%) sawa sawa na asilimia

NA	KILICHOPIMWA	USHIRIKI	WENYE UELEWA	ASILIMI A (%)	WASIO NA UELEWA	ASILIMI A (%)	KIWANGO CHA ELIMU			FANI	
							DEG	MASIT	TEKSO L	ELIMU	KISW
1	Uelewa juu ya maana ya Mikabala	7	6	86	1	14	1	5	2	1	3
2	Kutaja aina za Mikabala	7	3	43	4	57	-	3	2	-	1
3	Kuorodhesha aina za Mikabala	7	4	57	3	43	-	4	2	-	2
4	Uwiano wa Mikabala unaopima stadi moja na stadi Mchanganyiko	7	4	57	3	43	-	4	1	1	2
<b>WASTANI WA UJUMLA</b>		<b>7</b>	<b>4</b>	<b>57%</b>							

**Chanzo:** Uwandani (Agosti: 2020).

**NB:** Walimu wenye uelewa kuhusu mikabala ya utungaji mitihani ni asilimia 57% ambayo imepatikana kwa kuchukuliwa wastani ya washiriki wenye uelewa na kugawiwa kwa wastani wa idadi ya washiriki wote halafu ikazidisha kwa mia moja.

#### 4.2.1 Uelewa Juu ya Maana ya Mikabala

Katika kuchunguza ufahamu wawalimu kuhusu mikabala ya utungajimaswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Mtafiti alitaka kujua kama walimu hao wanauelewa juu ya maana ya mikabala ya utungaji mitihani ya lugha ambapo swali



kutoka katika dodoso liliuliza, nini maana ya mikabala ya utungaji mitihani ya lugha? Majibu ya swali hilo yalikuwa kama ifuatavyo: -

“Mikabala ya utungaji mitihani ya lugha ni utaratibu maalumu wanaotumia walimu wakati wa utungaji wa mitihaniya lugha”.

Katika kukitafutia majibu kipengele hiki, watoa taarifa saba walishiriki katika ujibuji wa dodoso la utafiti huu. Wataoa taari sita kati ya hao walionesha uelewa juu ya kipengele hiki ambao ni sawa na asilimia 86% ya washiriki wote.

Kwa upande wa viwango vyao vya elimu, watoa taarifa watono walikuwa na shahada ya uzamili. Kuhusu fani za elimu watoa taarifa wawili walikuwa na shahada ya uzamili ya ufundishaji Kiswahili kama lugha ya kigeni, watoa taarifa watatu walikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili na mtoa taarifa mmoja alikuwa na shahada ya kwanza ya ualimu.

Mtoa taarifa mmoja ambaye alikuwa na shahada ya uzamili ya ufundishaji Kiswahili kwa wageni hakuonesha uelewa kuhusu kipengele hiki cha maana ya mikabala ya utungaji mitihani ya lugha ambaye sawa na asilimia 14% ya watoa taarifa wote.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na watoa taarifa hao sita yalionesha ungaji mkono wa mawazo ya Canale na Swain (1980) pale waliposema kuwa mikabala ni mbinu ambazo hufafanua vipi mitihani inaweza kufanywa au kufanyika. Bachman (2010) anazidi kuliweka bayana swala hili kwa kusema kwamba inaminika kwamba wapimaji wa lugha ya pili/kigeni wana muunganyiko mmoja wa taaluma pamoja na ukuwaji wa maarifa ya ufahamu wa mambo yenye kuonesha utoaji tafsiri na muendelezo

wa matumizi ya upimaji. Mantiki ya maelezo haya ni kuonesha kwamba wapimaji wa lugha wanauelewa juu ya maana ya mikabala ya utungaji.

#### **4.2.2Kutaja Aina za Mikabala**

Katika kuchunguza ufahamu walionao walimu juu mikabala ya utungaji maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Utafiti huu ulichunguza uelewa wa walimu juu ya aina za mikabali ya utungaji mitihani ya lugha ya kigeni, kama swali lilivyojitokeza katika dodoso la utafiti huu. Kuna aina ngapi za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha? Majibu ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo; “Kuna aina mbili za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha”.

Watoa taarifa walionesha uelewa juu ya aina za mikabala walikuwawatatu ambao sawa na asilimia 43%. Watoa taarifa wote watatu walikuwa na shahada ya uzamili, wawili walikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya ufundishaji Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine na mmoja alikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili, kwa mujibu wa uchambuzi wa data ilioneka kwamba wenye fani ya ufundishaji Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine walikuwa nauelewa zaidi juu ya aina za mikabala kuliko wale wenye fani ya Kiswahili na wenye fani ya ualimu hawakuonesha uelewa wao kuhusu aina za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha.

Watoa taarifa ambao hawakuonesha uelewa wa kuhusu kipengele cha aina za mikabala ya utungaji mitihani walikuwa wanne ambao sawana asilimia 57%. Watoa taarifa wawili walikwana shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili, mmoja alikuwa na shahada ya uzamilia katika fani ya ualimu na mwengine alikuwa na shahada ya kwanza ya ualimu.

Kwa mujibu wa takwimu hizi inaonekana uelewa wa walimu juu ya aina za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha sio mkubwa. Tran (2012) kupitia utafiti wake ujuwilikanao kwa jina la upimaji wa lugha ya pili kwa walimu madarasani, kazi ambayo aliifanya katika Chuo Kikuu Cha Teknolojia ya Sayansi Nchini Marekani anasema kwamba elimu ya misingi ya upimaji na namna ya upimaji wa lugha nikitu kinachohitaji kuendelezwa kwa walimu wa lugha. Kwani ni vizuri mitihani wa lugha unaotungwa ukawa umeelekea katika mkabala fulani wa utungaji mitihani ya lugha (Oller na Richard, 1973). Maelezo haya yanazidi kuonesha kwamba elimu ya upimaji kwa walimu wa lugha ni kitu chenye umuhimu na cha ulazima.

#### **4.2.3 Kuorodhesha Aina za Mikabala**

Katika kuchunguza ufahamu walionao walimu juu mikabala ya utungaji maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Mtafiti aliwataka watoa taarifa waorodheshe aina za mikabala, ikiwa ni sehemu ya kutaka kujuwa ufahamu wao juu ya mikabala ya utungaji wa mitihani ya lugha. Watoa taarifa walionesha uelewa wao kuhusu kipengele hiki walikuwawanne ambao sawa na asilimi 57%. Majibu ya watoa taarifa hao yalikuwa hivi “mkaba unaopima stadi nyingi na mkabala unapima stadi moja kwa wakati mmoja”

Watoa taarifa wenye shahada ya uzamili katika fani ya ufundishaji Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine walikuwa wawili na wenye shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili walikuwa wawili. Kwa mujibu wa takwimu hizi utafiti ulionesha wazi kwamba ufahamu wa walimu kuhusu aina za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha

kwa watoa taarifa waliokuwa na fani ya ufundishaji Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingine pamoja na watoa taarifa waliokuwa na fani ya Kiswahili ni wenye kulingana na kwa upande wa watoa taarifa wenye fani nyingine za elimu hakukuwa na majibu yeyote.

Watoa taarifa ambao hawakuonesha uelewa wao katika kuorodhesha aina za mikabala walikuwa watatu ambao sawa sawa na asilimia 43%, kati ya hao waliokuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili walikuwa watoa taarifa wawili na mtoa taarifa mmoja alikuwa na shahada ya kwanza ya ualimu.

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kutoka kwa watoa taarifa hawakuenda kinyume na Oller na Richard (1973) pale waliposema kuwa kuna mikabala ya aina mbili mkabala unaopima stadi moja kwa wakati mmoja na mkabala unaopima stadi mchanganyiko kwa wakati mmoja. Hali hii ilionyesha kwamba walimu wanaofundisha Kiswahili kama lugha ya Kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar wanao uelewa katika kuorodhesha aina za mikabala ya utungaji mitihani ya lugha.

#### **4.2.4 Uwiano wa Mkabala Unaopima Stadi Moja na Stadi Mchanganyiko.**

Mtafiti wa utafiti huu aliwataka watoa taarifa waonesha uwiano uliopo baina ya mkabala unaopima stadi moja kwa wakati mmoja na mkabala unaopima stadi mchanganyiko kwa wakati mmoja. Ikiwa ni sehemu ya kuchunguza ufahamu walionao walimu juu mikabala ya utungaji maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kupitia dodoso la utafiti swali liliulizwa kama ifuatavyo: -

Mkabala unaopima stadi moja ya lugha kwa wakati mmoja unawiyana vipi na mkabala unaopima stadi mchanganyiko?

Majibu ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: -

“Mikabala yote miwili inafanya kazi ya kumtathimini mwanafunzi kuhusu kile alichosomeshwa katika lugha”

Watoa taarifa walioonesha uelewa kuhusu kipengele hiki walikuwa wanne ambao sawa na asilimia 57% ya watoa taarifa wote. Watoa taarifa wote wanne walikuwa na shahada ya uzamili, mtoa taarifa mmoja alikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya ufundishaji Kiswahili kwa wazungumzaji wa lugha nyingi, Mtoa taarifa mwengine alikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya ualimu na watoa taarifa wawili wengine walikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa takwimu hizi ilionekana wazi kwamba watoa taarifa wenye fani ya Kiswahili walikuwa na uelewa mzuri katika uwiyo uliopo baina mkabala unaopima stadi moja ya lugha na mkabala unaopima stadi mchanganyiko kwa wakati mmoja.

Watoa taarifa wasionesha uelewa kuhusu kipengele hiki walikuwa watatusawa na asilimia 43% ya watoa taarifa wote, ambapo mtoa taarifa wa kwanza alikuwa na shahada ya uzamili ya ufundishaji Kiswahili kama lugha ya kigeni, mtoa taarifa wa pili alikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili na mtoa taarifa wa mwisho alikuwa na shahada ya kwanza ya ualimu.

Kwa ujumla katika ukusanyaji majibu kwa ajili ya swali la kwanza la utafiti huu. Swali ambalo lilichunguza ufahamu wa walimu juu ya mikabala ya utungaji mitihani ya lugha. Utafiti ulionesha kwamba, watoa taarifa walionesha ufahamu waokuhusu swali hili ni wastani ya watoa taarifa wanne ambao sawa na asilimi 57%. Kwa asilimia hii ilionekana wazi kwamba ufahamu walionao walimu kuhusu mikabala ya utungaji mitihani ulikuwa wa kuridhisha. Pia majibu yao yalikuwenda sambamba na nadharia ya tabia ya umoja

(Unitary Trait Hypothesis) iliyotumika katika utafiti huu. Kwani kwa mujibu wa nadharia hii, ilielezwa kwamba elimu ya mikabala ya utungaji mitihani ya lugha ni kitu cha msingi, pia ni jambo lilopewa kipaumbele cha hali ya juu (Oller, 1979).

### 4.3 Mkabala Unaotumika Zaidi Katika Utungaji wa Maswali ya Mitihani

Kupitia swali la pili la utafiti huu, mtafiti alitaka kujua mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Katika kulitafutia ufumbuzi swali hili mtafiti alitumia mbinu ya dodoso na mbinu ya uchambuzi wa nyaraka kama njia za ukusanyaji wa data.

Kwa kuanzia na njia ya dodoso, mtafiti wa utafiti huu aliuliza swali lifuatalo katika ukusanyaji wa data za lengo la pili kama linavyoonekana; Bainisha mkabala unaotumitua zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kwa wageni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar?

Majibu ya data ambazozilikusanywa kwa njia ya dodoso zilikuwa kama ifuatavyo: -

#### Jadweli 1.2

#### *Makabala Unaotumika Zaidi Katika Utungaji wa Maswali ya Mitihani*

**Ufunguo:** Ufafanuzi wa vipengele vya jadweli hili ni sawa sawa na ule uliotolewa katika jadweli la pili hapo juu.

NA	KILICHOPIMWA	USHIRIKI	WALIOJIBU SAHIHI	WASIJIBU SAHIHI	KIWANGO CHA ELIMU				FANI	
					DEG	MAST	PHD	TEKSOL	ELIMU	KISW
1	Makabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani	7	6	1	1	5	-	2	1	3

**Chanzo:** Uwandani (Agosti: 2020).

Watoa taarifa sita walionesha uelewa wao kuhusu kipengele hiki, watoa tarifa wawili kati ya hao walikuwa na shahada ya uzamili ya ufundishaji Kiswahili kwa wageni, mtoa taarifa mmoja alikuwa na shahada ya kwanza ya elimu na watoa taarifa watatu walikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili na mtoa taarifa mmoja aliyekuwa na shahada ya uzamili katika fani ya ualimu hakuonesha uelewa wake kuhusu kipengele hiki.

Watoa taarifa waliotowa majibu kuhusu swali hili, walisema kwamba “mkabala unaotumika zaidi ni mkabala unaopima stadi nyingi kwa wakati mmoja” Ambapomajibu ya watoa taarifa hao yalikuwenda sambamba na mtazamo wa nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Trait Hypothesis) pale iliposema, umahiri wa lugha ni kitu kinachopimwa katika muunganyiko zaidi, kuliko kupimwa katika hali ya kutenganiswa (Oller, 1979).

Kwa mujibu wa Alhsussein (2009) upo umuhimu wa kuipima lugha pasina kuiacha stadi hata moja katika stadi zake kuu. Kwani kwa kawaida mkabala mjumuishi humsaidia mjifunzaji wa lugha ya kigeni kupata muda mkubwa wa kufanya mazungumzo na kuweza kuitumia lugha katika mazingira yake ya kawaida nje ya mazingira ya kujifunza baada ya kuzihitimu stadi za lugha inayohusika. Kwa sabababukila siku lugha huhitajika kupimwa kwa namna ambayo wajifunzaji wataweza kuitumia nje ya mazingira ya darasani (Moeller na Catalano 2015).

#### **4.3.1 Uchambuzi wa Mitihani ya Kiwango Cha Kati ya Mwaka 2017**

Mitihani ya mwaka 2017 iliyofanyiwa uchambuzi ni yale ya tarehe 29/09/2017 na tarehe 13/12/2017.

**a) Mtihani wa Kiwango Cha Kati wa Tarehe 29/09/2017**

Mtihani huu ulikuwa na maswali tisa.

**Swali Nambari: 1**

Swali hili lilikuwa ni swali la ufahamu, swali ambalo ndani yake lilikuwa na maswali madogo madogo, maswali ambayo majibu yake yalitegemewa kupatikana kutoka katika ufahamu kwa hivyo maswali haya ni maswali ya ufahamu, swali hilo kwa ujumla wake lilikuwa kama ifuatavyo: -

**Mfano Nambari: 1**

**1. Soma ufahamu na baadae ujibu maswali yanayofuata chini**

Mfumo wa maisha ya jamii hivi sasa ni mfumo unaotawaliwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya fedha. Namna moja wapo ya wanajamii kupata fedha ni kupitia kuajiriwa. Zipo ajira rasmi na ajira zisizo rasmi. Ajira rasmi ni kama vile uaskari, udaktari, ualimu, udereva. Ajira zisizo rasmi ni kama vile uuzaji wa matunda na mboga mboga, uendeshaji wa duka au mkahawa, kufanya vibarua mashambani na ushonaji.

Mfumo huu wa maisha umesababisha si tu watu wazima kufanya kazi hizo mbali mbali ili kujipatia fedha, bali pia watoto wengi wameingizwa kwenye ajira, hasakatika mfumo wa ajira zisizo rasmi. Watoto wengi wanafanya kazi kwenye migodi, kama vile ya dhahabu na tanzanaiti; kwenye mashamba, kama vile ya chai, kahawa na pamba; kwenye kazi za majumbani, kama vile kulima, kufua, kupika na kuchunga mifugo; kwenye upasuaji wa mbao n.k.

Ziko hasara nyingi zinazotokana na kitendo cha kuajiri watoto. Kukosa fursa ya kupata elimu ni hasara mojawapo kubwa. Wapo watoto wengi ambao wameacha shule ili waweze kwenda kufanya kazi za kuajiriwa. Hasara nyingine ni kuathirika kwa ukuaji wao. Kuna watoto wengi ambao umri wao ni mdogo, lakini wanafanyishwa kazi nzito mno. Kazi hizo ni kama vile kupasua mbao, kuvunja kokoto na kuvunja mawe yenye madini migodini. Hizi ni kazi ambazo



haziendani na umri wao, hivyo huelemewa miili yao ambayo bado ni michanga na kuifanya isikue sawa sawa.

Vile vile watoto wengi hudhulumiwa hata kiasi kile kidogo cha malipo ambacho waliahidiwa kulipwa na hao waajiri wao. Pale wanapodai malipo yao, hufukuzwa. Hatima yake ni kukosa namna ya kujikimu kimaisha, hivyo kujiingiza katika makundi ya watoto wa mitaani na kuanza kutumia dawa za kulevya na hata kufanya ukahaba. Hasara nyingine ni kutengwa na familia zao, mathalani hutolewa vijijini na kupelekwa mijini, watoto hao hukosa malezi ya wazazi, hivyo hutumbukia kirahisi katika makundi ya kihalifu, kama vile ujambazi na uvutaji bangi. Tufanyeje ili kuepukana na tatizo la ajira kwa watoto? Kwanza serikali kutunga na kusimamia sheria zinazopiga marufuku ajira kwa watoto. Pili ni muhimu kuelimisha umma juu ya athari zinazoambatana na kuwaajiri watoto, maana watu wengine huwaajiri watoto au kuruhusu watoto waajiriwe. Serikali iinue kipato cha kawaida, kwa mfano kwa kutoa ruzuku za mbolea, ili watu wa weze kumudu mahitaji ya msingi ya familia.

### **Mfano wa Baadhi ya Maswali Yalioulizwa**

- a) Unafikiri kuna tafauti gani kati ya ajira rasmi na ajira zisizo rasmi?
- b) Eleza hasara mbili wanazozipata watoto kutokana na kuajiriwa?
- c) Kulingana na habari uliyoisoma, taja mambo mawili ambayo yanaweza kusaidia kuondoa tatizo la ajira kwa watoto?

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kwanza aisome habari na aifahamu akisha ajibu maswali yaliyoorodheshwa chini yake. Kwa mujibu wa swali hili stadi mbili za lugha ndizo zilizopimwa. Kwanza stadi yakusoma kwa kumtaka mwanafunzi aisome habari na stadi ya kuandika kwa kumtaka mwanafunzi ajibu maswali baada ya kwisha kuisoma habari hiyo Oller (1979) kupitia nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Trait Hypothesis) ambayo ilitumika katika utafiti huu inasemakwamba, umahiri wa lugha ni kitu kinachopimwa katika muunganyiko zaidi kuliko kupimwa katika hali ya kutenganiswa. Oller (1979) amekwenda mbali zaidi kwa kusema kwamba, kuna sifa za

ujumla kuhusu umahiri wa lugha, ambapo mkabala unaopima stadi za lugha kwa kuzitenganisha au kuzibagua si miongoni mwa sifa hizo (Oller, 1979).

Hali hii ilioneshakwamba nadharia iliyotumika katika utafiti huu ilikwenda sambambana kazi husika. Alhussain (2009) kupitia utafiti wake alioufanya Chuo Cha Kimataifa Cha Sayansi ya Afya kilichopo Riyadh, Saudi Arabia anasema inapendeza zaidi ikiwa lugha itasomeshwa na kupimwa katika hali ya mjumuishi. Lakini Bell (1981) na Harri (1969) wanaeleza kwamba lazima mitihani ipime kile ambacho inatakiwa kukipima.

Ikiwa hali iko hivyo, ni wazi kwamba swali la ufahamu ambalo mwanafunzi ametakiwa kulijibu kwa kuisoma habari akisha ayajibu maswali litakuwa ni lenye kuleta changamoto kwa mpimaji kwani katika mchakato mzima wa kuandika, ikitokea mwanafunzi kashindwa kuandika majibu si rahisi mpimaji (mwalimu) kuweza kufahamu kwamba mwanafunzi huyo anaudhaifu katika stadi ipi ya lugha.

Jee, udhaifu wake upo katika stadi ya kusoma kwa hivyo ndio maana alishindwa kuandika kwa sababu hakuifahamu habari au habari aliifahamu lakini alishindwa kuandika kwa sababu hajuwi kuandika. Heaton (1998) anafafanua katika kitabu chake kinachozungumzia mitihani ya lugha amesema kwamba ubora wa mitihani uko kwenye kile ambacho unasitahiki kukipima na sichengine chochote.

**Swali Nambari: 9**

Swali la tisa la mtihani huu lilikuwa swali la utungaji wa Insha ambapo mwanafunzi alitakiwa kuchagua mada moja kisha aitungie insha, swali hilo lilikuwa kama ifuatavyo:

-

## **Mfano Nambari: 2**

### **Tunga insha kwa kutumia mada ifuatayo**

- a) Uchafuzi wa mazingira Zanzibar.

Swali hili lilimtaka mwanafunzi atunge insha kutokana na mada aliopewa. Katika uchambuzi wa swali hili mtafiti aligundua kwamba stadi ya lugha iliyokuwa ikipimwa ni stadi moja tu, nayo ni stadi ya kuandika.

Kwa uwazi kabisa mada ambayo mwanafunzi alitakiwa kuitungia insha ilihusu maisha halisi kama zilivyo mada nyingine za maswali kama hili kutoka katika mitihani yote yaliochambuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Mada aliotakiwa mwanafunzi kuitungia insha pamoja na majibu yaliopatikana katika mchakato mzima wa uchambuzi wa nyaraka yalikuwenda sambamba na nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Trait Hypothesis) kama ilivyotumika katika utafiti huu. Oller (1979) anaeleza kwamba taaluma ya sarufi tarajiwa imeonesha umuhimu zaidi juu ya ukweli kwamba muunganyiko wa vipengele na madaraja yake, ambavyo vinaitengeneza lugha ni vyenye kupatikana kwa watumiaji wa lugha katika mazingira halisi ya kimaisha. Hii ni kwa sababu kwa namna fulani yameunganishwa na mazingira ya ziada ya kilughawiya yenye kufaa (Oller, 1986).

Jambo hili liliaonesha wazi kwamba kuna umuhimu mkubwa kwa mitihani ya lugha kupima uwezo wa kuitumia lugha katika mazingira halisi ya kila siku (Cohen 1994). Hivyo basi, majibu yaliyopatikana kupitia utafiti huu na nadharia iliyotumika ni vitu vyenye kukamatana.

**b) Mtihani wa Kiwango Cha Kati wa Tarehe 13/12/2017**

Mtihani huu uligawiwa katika sehemu tano kutoka sehemu “A” hadi sehemu “E”, katika mtihani huu mtafiti alifanya uchambuzi kwa kulizingatia swali la sehemu “A” na sehemu E. Sehemu “A” ilikuwa na maswali tisa yaliohusiana na ufahamu ambapo ndani yake kulikuwa na upimaji wa stadi ya kusoma na stadi ya kuandika.

Sehemu “E” ya mtihani huu ilikuwa na swali lililopima stadi ya kuandika kwani lilikuwa swali la utungaji wa insha. Maswali hayo yalichambuliwa kama ifuatavyo: -

**Sehemu “A”:** Swali la sehemu hii lilikuwa kama ifuatavyo: -

**Mfano Nambari: 3**

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yafuatayo: -**

Uchumi wa Tanzania unategemea sana kilimo. Sekta ya kilimo inachangia karibu nusu ya **mapato** ya taifa. Uzalishaji katika kilimo unapanda na kushuka kwa kasi kutoka na mabadiliko ya tabia nchi na upungufu wa nishati na mashine. **Sera** ya serikali kwa kilimo inahimiza kilimo cha mazao ya chakula kama mahindi, muhogo, mtama, uwele, mpunga, ndizi, majimbi, viazi n.k.

Kwa upande mwingine, kuna mazao ya biashara kama karafuu, nazi, pili pili hoho na **mwani** kwa Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania bara mazao ya biashara ni kama pamba, mkonge, korosho, chai, tumbaku n.k

Hata hivyo, pamoja na kuwepo sera hii, bado upungufu wa chakula unatokea kwa baadhi ya vipindi. Mazao yanayouzwa nchi za nje huipatia nchi yetu fedha nyingi za kigeni. Mbali na vyanzo hivyo, Tanzania inapata fedha za kigeni kwa kupitia vyanzo vingine vya madini. Kuna madini mengi yanayozalishwa Tanzania miongoni mwa hayo ni almasi, dhahabu, chuma n.k Tanzanite nimadini yanayopatikana Tanzania pekee. Pia kuna uwezekano mkubwa wa Tanzania kuchimba madini ya Urenium. Haya ni madini muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda na ni chanzo cha umeme wa uhakika. Pia gesi asilia **imegunduliwa** kwa wingi ukanda wa bahari ya kusini katika visiwa vya Songo songo. Gesi hii imeshaanza kuchimbwa na tayari imeanza kutumika kama ni moja kati ya vyanzo vya umeme nchini Tanzania.

Viwanda kwa upande wake, vinachangia **asilimia** ndogo ya pato la taifa na kuajiri **nguvu kazi** ndogo ya watanania. Viwanda hivi vimemilikiwa na mashirika ya watu binafsi na hivyo **kuzalisha** bidhaa mbali mbali za matumizi ya ndani kama vile nguo, viatu, usindikaji wa matunda, maziwa n.k. Viwanda hivi hutumia malighafi za ndani ya nchi kama vile pamba, ngozi, n.k. Tanzania inautajiri mkubwa wa maji ya mito na maziwa yanayotumika katika uzalishaji wa umeme unaotumika katika viwanda vidogo vidogo. Asilimia sabini (70%) ya viwanda vidogo vidogo vinatumia nishati ya umeme wa maji.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea, inaagiza bidhaa mbali mbali kutoka **ughaibuni**, miongoni mwa bidhaa hizo ni pamoja na mafuta ya petrol na dizeli, mitambo na mashine za viwandani, madawa, magari, ndege n.k. Hakuna uwiano kabisa wa bidhaa zinazozalishwa ndani na zinazouzwa nje. **Gharama** ya bidhaa zinazo agizwa nje ni kubwa mara mbili kuliko zile zinazozalishwa nchini nakusafirishwa nchi za nje. Hii inamaanisha kuwa Tanzania inatumia fedha nyingi za kigeni kuagizia bidhaa kutoka nje. Tanzania inafanya biashara na mataifa mbali mbali duniani kama Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Ulaya na Uingereza, Marekani, nchi za Asia na Mashariki ya mbalikama vile, Malaysia, China, Korea ya Kaskazini, Japani, India n.k.

Sehemu nyingine inayochangia mapato katika uchumi wa Tanzania ni sekta ya utalii. **Sekta** hii ilitambuliwa rasmi kama ni muhimu katika kukuza uchumi wa taifa katika miaka ya 90. Kuanzia hapo hoteli za kitalii zilishamiri kila penye ufukwe na mbuga katika Tanzania. Idadi ya watalii imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Hivi sasa utalii ni chanzo muhimu cha mapato na kinachotegemewa katika kukuza uchumi wa taifa.

Visiwa vya Zanzibar vimekuwa maarufu duniani licha ya kuzalisha karafuu zenye ubora duniani, uzuri wa fukwe kumewafanya watalii **kumiminika** kwa mamia kutoka pembe zote za dunia. Sekta ya utalii kwa Zanzibar ni chanzo cha pili kinachoingiza fedha za kigeni badala ya karafuu.

### **Mfano wa Baadhi ya Maswali Yalioulizwa**

1. Eleza umuhimu wa sekta ya kilimo katika kukuza uchumi wa Tanzania.
2. Ungependekeza Zanzibar ifanye nini katika kukuza zaidi sekta ya utalii?
3. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi mia moja.

Kupitia swali hili mwanafunzi alitakiwa kuisoma habari kwa umakini na aifahamu baada ya hapo ajibu maswali yaliorodheswa chini ya habari. Kwa mantiki hiyo maswali yote ya sehemu hii kutoka swali la kwanza hadi swali la tatu, yalikuwa maswali ambayo yanapima stadi mbili za lugha yaani stadi ya kusoma na stadi ya kuandika. Kwani mwanafunzi alitakiwa kuisoma habari vizuri na kwa umakini akimaliza ajibu maswali kwa njia ya maandishi. Maelezo haya yaliungwa mkono na nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Trait Hypothesis) kama ilivyotumika katika utafiti huu. Wakati wa upimaji wa lugha kuna umuhimu mkubwa wa kuzikusanya pamojo stadi kuu za lugha katika upimwaji wake (Oller, 1979).

**Sehemu “E”:** Sehemu hii ilimtaka mwanafunzi achaguemada moja kati ya mada zilizo rodheshwa akisha andike insha isiyopungua maneno 100 juu ya mada atakayoichagua. Swali lenyewe lilikuwa kama ifuatavyo: -

**Mfano Nambari: 4**

Andika Insha isiyopungua maneno 100 juu ya mada zifuatazo

1. Nilipokuwa mtoto. 2. Nitakaporudi kwetu. 3. Maisha yangu Zanzibar
4. Matarajio yangu baada ya kumaliza masomo. 5. Tukio nisilolisahau maishani mwangu.

Sehemu “E”. Sehemu hii ilikuwa na mada tano za kuandika insha mada zote kwa ujumla wake zilikuwa na uwezo wa kumpima mwanafunzi stadi moja ya lugha. Stadi yenyewe ni stadi ya kuandika kwani mwanafunzi alilazimika kuzisoma kidogo tu ili azifahamu. Lakini kazi zaidi ilikuwa katika uandishi ambapo mwanafunzi alitakiwa kuitumia akili vizuri katika kuhakikisha kwamba anachokiandika kitaendana na mada husika kwa kuzingatia mazingira halisi ya matumizi ya lugha.

Bachman (1991) anaeleza kwamba katika mtihani wa lugha neno mazingira halisi inatafsirika kama ni hali ambayo yale yaliyomo katika mitihani pamoja na masharti yake yote yawe yamelenga katika mazingira ya maisha ya kawaida. Naye Ramadan (2020) dhana ya mazingira halisi inamaanisha kwamba lugha inahitaji wanafunzi wapewe mitihani inayohusiana na mawasiliano ya lugha ya kila siku. Haya yote ni mambo ya msingi kabisa kama yalivyoelezwa na nadharia ya tabia ya umoja iliyotumika katika utafiti huu (Oller, 1979).

### **4.3.2 Uchambuzi wa Mitihani ya Kiwango Cha Kati ya Mwaka 2018**

Mitihani ya mwaka 2018 iliyofanyiwa uchambuzi ni ule ulifanywa tarehe 24/08/2018 na ule uliofanywa tarehe 06/09/2017.

#### **a) Mtihani wa Kiwango Cha Kati wa Tarehe 24/08/ 2018**

Mtihani huu ulikuwa na maswali tisa, maswali ambayo yalibeba maswali madogo madogo yenye maelekezo tofauti.

#### **Swali Nambari: 1**

Swali hili lilikuwa ni swali la ufahamu, swali ambalo lilimtaka mwanafunzi kuisoma habari akisha ayajibu maswali aliyoulizwa ambapo yalikuwa ni kuanzia swali la (a) hadi swali la (i). Pia swali la (i) lilikuwa na maswali mengine madogo madogo ambayo ni swali la kwanza hadi swali la nne. Swali hili la ufahamu kwa ujumla wake lilionekana kama ifuatavyo: -

#### **Mfano Nambari: 5**

#### **Soma habari hii na kisha ujibu maswali yafuatayo.**

Mimi ni mwalimu wa lugha na fasihi katika shule ya msingi ya Kilimani mjini Nairobi. Ninaishi mtaa wa Buruburu ambao uko mashariki mwa jiji la Nairobi. Kazi yangu huanza saa moja na dakika kumi na tano asubuhi hadi saa kumi na nusu kila siku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Jumamosi na Jumapili mimi hupumzika.

Nikitaka kufika shuleni wakati mzuri kabla ya saa moja na robo, ni lazima niamke mapema. Kwa hivyo saa yangu huniamsha saa kumi na mbili kamili kila siku. Mimi hujiandaa katika muda wa dakika ishirini. Kituo cha basi hakiko mbali na nyumba yangu na kwa hivyo mimi huchukua basi la saa kumi na mbili na dakika ishirini na tano. Basi



hili huvuka mji na hunishusha umbali wa mita mia mbili kutoka shuleni ninapofanya kazi.

Wakati huo huwa kama saa moja na kasoro dakika kumi. Ikiwa kwa bahati mbaya basi hili limeniacha mimi hulazimika kupanda matatu hadi kati kati mwa mji halafu huchukua matatu nyengine hadi shuleni. Ni ghali zaidi kupanda matatu mbili na kwa hivyo mimi huhakikisha ya kwamba nimeliwahi lile basi la asubuhi. Jioni mimi huwa sina haraka sana kama asubuhi na huanza safari yangu ya kurudi nyumbani kama saa kumi na moja kasoro dakika ishirmi. Nikichukua basi la wakati huu, mimi hufika nyumbani saa kumi na moja na nusu, wakati mzuri wa kupika chai na kumpumzika kabla ya kuanza shughuli za jioni.

Kwa sababu hakuna haja ya kupanda usafiri wakati wa wikiendi mimi hulala hadi saa tatu halafu ninaamka na kuanza shughuli zangu za wikiendi.

### **Mfano wa Baadhi ya Maswali Yalioulizwa**

- a. Kutokana na makala haya, mwandishi anapenda kutumia matatu au basi kwenda shule, kwa nini?
- b. Mwandishi hufanya nini anaporudi kutoka shuleni?
- c. Tunga sentensi nne (4) kwa kutumia msamiati

1) Makala    2) Hakikisha    3) Chukua    4) Jiandaa

Kwa mujibu wa swali la ufahamu la mtihani huu na kwa namna ya lilivyoulizwa pamoja na kazi ambayo mwanafunzi alitakiwa kuifanya bila ya shaka swali hili lilipima stadi mbili za lugha, stadi ya kusoma na stadi ya kuandika kwa sababau mwanafunzi alitakiwa kuisoma habari akimaliza ayajibu maswali aliyoulizwa.

Wakati mwanafunzi alipoisoma habari alikuwaanapimwa stadi ya kusoma na wakati alipokuwa anajibu maswali yaliyoorodheshwa chini ya habari alikuwa anapimwa stadi ya kuandika. Kwa hivyo swali hili lilipima stadi mbili za lugha kwa wakati mmoja kama

nadharia ya tabia ya umoja (Unitary traty Hypothesis) ilivyopendekeza juu ya umuhimu wa kuipima lugha kwa kuzingatia stadi nyingi za lugh kwa wakati mmoja (Oller, 1979).

**Swali Nambari: 9**

Swali la tisa la mtihani huu lilikuwa swali la utungaji, swali ambalo lilimtaka mwanafunzi andike habari kutokana na moja kati ya mada alizopatiwa, mada hizo zilikuwa kama ifuatavyo: -

**Mfano Nambari: 6**

**Andika habari kuhusu moja kati ya mada zifuatazo:**

- a. Maisha ya Ujerumani.
- b. Nitakaporudi Ujerumani.

Kwa mujibu wa maelekezo ya swali hili mtafiti aligundua kwamba mwanafunzi alikusudiwa kupimwa uwezo wake wa kutunga insha kutokana na mada alizopewa. Kwa hivyo, kupitia swali hili mtafiti alipata majibu ya kwamba mwanafunzi alikuwa anapimwa stadi ya kuandika tu. Stadi hiyo ilichukuwa nafasi kubwa zaidi katika ufanyaji wa kazialiyoelekezwa mwanafunzikuifanya, ingawa ilionekana wazi kwamba mwanafunzi hawezi akatunga insha kama hajazisoma mada na kuzifahamu baada ya hapo akaendelea na mchakato wa utungaji kama alivyoelekezwa kwenye swali la mtihani.

Ukizichunguza mada alizotakiwa mwanafunzi kuzitungia insha kwenye swali hili ni mada ambazo zilijikita katika mazingira ya kawaida ya maisha ya watumiaji wa lugha. Kama walivyoieleza Bachaman na Palmer (1996) pale waliposema mitihani yanayozingatia mazingira, huwa yanajaribu kuweka ukaribu wa mazingira halisi ya maisha kadri ya inavyowezekana. Wazo hilo linaenda sambamba na ufafanuzi wa nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Treaty Hypothesis). Oller (1986) anaeleza kwamba jambo hili ni muhimu kwa sababu madaraja ya vipengele vya lugha yameunganishwa na mazingira ya ziada ya kilughawiya yenye kufaa.

**b) Mtihani wa Kiwango Cha Kati wa Tarehe 06/09/ 2018**

Mtihani huu ulikuwa na maswali tisa. Kwa mujibu wa stadi za lugha ambazo mtafiti alizizingatia katika uchambuzi wake, maswali mawali ya mtihani huu ndiyo yaliochambuliwa, nayo ni swali la kwanza na swali la pili. Maswali hayo yalikuwa kama ifuatavyo: -

**Swali Nambari: 1**

Swali la kwanza la mtihani huu lilikuwa ni swali la ufahamu. Swali ambalo lilimtaka mwanafunzi kuisoma habari akisha ayajibu maswali yalioainishwa, swali hili lilikuwa limebebe maswali mengine madogo madogo sita kutoka (a) hadi (f) kama ifuatavyo: -

## **Mfano Nambari: 7**

### **Soma habari hii kisha jibu maswali**

Mkurugenzi wa Shirika la Makazi Duniani (UN Habitat) Profesa Anna Tibaijuka ambaye amewataka wananchi wenzake hasa wanawake kufanya kazi kwa bidii na kuacha tabia ya kuwalalamikia waume zao wanapokosa maendeleo. Alisema kila mwanamke ana jukumu la kufanya kazi kwa bidii na kwamba wasitegemee kuletewa maendeleo na mtu mwengine. Alisema maneno hayo jijini Dar es Salaam alipokutana na wanawake wanaotoka kijiji cha Maruku mkoa wa Kagera.

Profesa Tibaijuka aliwaambia wanawake hao kwamba kama wakiwezesha wanaweza kufanya mambo makubwa katika maisha yao na kuzisaidia familia zao. Alisema jukumu la kwanza la kulea watoto ni la mama na asipojitahidi anaweza kuiangusha familia nzima. Aliwalaumu wazazi kwa kushindwa kuwasomesha watoto wa kike hatua ambayo alisema imewafanya wawe nyuma kielimu na hivyo kuwafanya wakose maendeleo.

Aliongeza kwa kusema kuwa yeye alifanikiwa kusoma kutokana na wazazi wake kuwa na uwezo wa kumwezesha kwenda shule. Akizungumza katika mkutano huo mwenyekiti wa kikundi cha wanawake hao kinachojulikana kama “Maruku Tunaweza” Dkt. Emelia alisema njia pekee ya kuwakomboa wanawake ni wao wenyewe kuungana na kufanya kazi kwa bidii. Alisema kikundi hicho kinajumuisha wanawake wanaotoka katika kijiji cha Maruku na malengo yao makubwa ni kutafuta njia za kujikomboa na umasikini.

### **Mfano wa baadhi ya maswali yalioulizwa**

- a) Kikundi cha “Maruku Tunaweza” kina watu wa aina gani?
- b) Profesa Anna Tibaijuka aliwaambia wananchi nini?
- c) Aliwalaumu nani na kwa nini?
- d) Kwa nini yeye alifanikiwa na yeye sasa ni nani?

Kwa mujibu wa swali hili mwanafunzi ili aweze kuzitungia insha mada hizi kwanza alitakiwa kuisoma habari na kuifahamu halafu ndipo aweze kuyajibu maswali kwa usahihi. Kwa mujibu wa nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Traty Hypothesis) inaonekana wazi kwamba katika swali hili mwanafunzi alipimwa stadi ya kusoma pamoja na stadi ya kuandika, ambapo mkabala unaopima stadi nyingi kwa wakati

mmoja ndio uliotumika kwa sababu ndani yake kuna stadimbili za lugha zilizopimwa kwa wakati mmoja (Oller, 1979).

### **Swali Nambari: 9**

Swali hili lilikuwa ni swali la utungaji. Swali ambalo lilijitokeza katika mtihani kama ifuatavyo: -

### **Mfano Nambari: 8**

Andika kuhusu ziara uliyoipenda na ueleze kwa nini uliipenda na ulijifunza nini na mambo ambayo yalikuwutia katika ziara hiyo. (Maneno200).

Swali la tisa la mtihani huu lilijikita zaidi katika stadi ya kuandika kwani lilimtaka mwanafunzi kuandika kuhusu ziara aliyopenda lakini pia lilihusiswa na mazingira halisi ya mwanafunzi. Swali hili liliendana nanadharia ya tabia ya umoja (Unitary Traty Hypothesis), kupitia nadharia hiyo Oller (1979) anafafanuakwa kusema kwamba lugha hupimwa kwa mujibu wa mazingira ya watumiaji wake.

Wakati wa ujibuji wa swali hili kazi kubwa aliyofanya mwanafunzi ilikuwa ni kuandika ikiwa ni sehemu ya utungaji. Kwa hivyo mwanafunzi alipimwa stadi ya kuandika wakati wa ujibuji wa swali hili lakuzingatia ni kwamba mjifunzaji wa lugha sio tu kwamba atengeneze miundo ya sentensi yenye usahihi kisarufi bali pia aweze kuitumia lugha kwa usahihi kwa mujibu wa mazingira ya kijamii(Spolsky 1975).

### **4.3.3 Uchambuzi wa Mitihani ya Kiwango Cha Kati ya Mwaka 2019**

Mitihani ya mwaka 2019 iliyofanyiwa uchambuzi ni ule ulifanywa tarehe 31/01/2019 na ule uliofanywa tarehe 20/09/2019.

#### **a) Mtihani wa tarehe 31/01/ 2019**

Mtihani huu ulikuwa na maswali nane, maswali ambayo ndani yake yalibeba maswali madogo madogo yenye maelekezo tofauti. Lakini kutokana na stadi za lugha zilizozingatiwa katika utafiti huu, mtafiti alifanya uchambuzi wa maswali mawili tu, swali la kwanza na swali la nne. Kwa kuanzia na swali la kwanza ni kama ifuatavyo:

#### **Swali Nambari: 1**

Swali hili lilikuwa la ufahamu, ambapo mwanafunzi alitakiwa kuisoma habari akisha ayajibu maswali yaliyoorodheshwa, ufahamu na maswali yake yalikuwa kama ifuatavyo: -

#### **Mfano Nambari: 9**

#### **Soma habari ifuatayo na kisha ujibu maswali yanayofuata:**

Mzee masika alikuwa anafuga mbwa nyumbani kwake. Mbwa huyo alikuwa mzuri na mwaminifu sana. Mzee masika na mbwa wake waliishi pamoja siku zote wote walipendana na walisaidiana.

Siku moja mzee masika alitaka kwenda dukani kununua unga wa sembe na mafuta ya taa. Nyumbani hakukua na mtu wa kukaa na kumlea mjukuu wake ambaye alikuwa mchanga. Hivyo alimuacha mbwa wake amlinde mtoto mchanga. Aliporejea kutoka dukani, Yule mbwa alimlaki mzee masika kwa furaha kubwa. Lakini kinywa chake kilijaa damu. Mzee masika alifikiri mbwa amemla mjukuu wake. Bila ya kufikiri alichukua shoka na kumkata kichwa masikini wee! Mbwa alikufa.

Baadaye aliingia ndani ili kumwona mjukuu wake aliyeliwa na mbwa. Alimkuta mzima na anacheza cheza juu ya kitanda chake. Lo! Kumbe mzee masika alimuuwa bure mbwa wake. Kuangalia mvunguni mwa kitanda cha mjukuu wake aliona joka kubwa, joka hilo lilikuwa limekufa liliraruliwa na kutoka damu tele ilionekana chini ya kitanda. Kumbe mbwa alimuuwa joka ili kumwokoia mtoto. Mzee masika alilia sana kwa kumuuwa mbwa wake bila ya sababu.

### **Mfano wa Baadhi ya Maswali Yalioulizwa**

- 1) Nani alikuwa anafuga mbwa
- 2) Nani alimuuwa mbwa?
- 3) Unafikiri kwa nini mbwa aliuliwa

Kwa mujibu wa swali hili la ufahamu, ili mwanafunzi aweze kulijibu lazima aisome habari kwa umakini na aifahamu. Baada ya mtafiti kuupitia ufahamu na kuyaangalia maswali yalioulizwa aligundua kwamba stadi za lugha ambazo zilikuwa zinapimwa kupitia swali hili ni stadi ya kusoma na stadi ya kuandika. Kwa mantiki hiyo swali hili lilikuwa la mkabala mjuishi kwani lilipima stadi nyingi kwa wakati mmoja. Hata Nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Traty Hypothesis) ambayo ilitumika katika utafiti huu ililisisitiza jambo hili kwa kusema kwamba lugha lazima ipimwe katika hali ya mjumuishi ili iweze kutoa umahiri mzuri kwa mjifunzaji (Oller, 1979).

### **Swali Nambari: 8**

Swali la nane la mtihani huu lilikuwa ni swali la kuandika, ambapo mwanafunzi alipewa mada nne ili achague mada moja kati ya hizo baada ya hapo atunge insha ya maneno 150-200. Swali lenyewe lilikuwa kama ifuatavyo: -

**Mfano Nambari: 10**

Chagua mada moja na Andika Insha isiyoziidi maneno 150-200

1. Nchi yangu. 2. Histori yako. 3. Maisha katika nchi yangu. 4. Siku ambayo sitoisahau.

Kwa mujibu wa muonekano wa swali hili mwanafunzi alitakiwa kuchagua mada moja akisha andike insha kuhusu mada hiyo. Kwa mnasaba wa swali hili mtafiti aligundua kwamba swali hili lilimpima mwanafunzi stadi ya kuandika kwa kiasi kikubwa. Wakati wa ujibuji wa swali hili mwanafunzi alitakiwa aitumie lugha kwa mujibu wa mazingira ya mada husika pamoja na mazingira halisi ya watumiaji wake (Kumar 2019).Ufafanuzi huu ulikwenda sambamba na nadharia ya tabia ya umoja (Unatary Traty Hypothesis), nadharia ambayo ilionesha umuhimu wa uzingatiaji mazingira halisi wakati wa ujifunzaji wa lugha na utungaji wa mitihani ya lugha hasa lugha ya kigeni (Oller, 1979).

**b) Mtihani wa Kiwango Cha Kati wa tarehe 20/09/ 2019**

Mtihani huu ulikuwa na sehemu mbili sehemu ya kwanza ambayo ilikuwa na swali la ufahamu na sehemu ya pili ilikuwa imejikita zaidi katika sarufi, ambapo ndani yake kulikuwa na swali la insha. Kwa hivyo, mtafiti wa utafiti huu alichambua maswali mawili tu katika mtihani huu swali la kwanza na swali la saba kwa mujibu wa stadi kuu za lugha alizokuwa anazingatia, kama ifuatavyo: -



**Swali Nambari: 1**

Swali hili lilikuwa lina mfumo wa ufahamu, swali ambalo mwanafunzi alilazimika kuisoma habari vizurina akifahamu kilichomo ndani yake akimaliza ayajibu maswali yalioorodheshwa chini ya ufahamu huo, ufahamu pamoja na maswali yake yalikuwa kama ifauatavyo: -

**Mfano Nambari: 11****Soma habari hii kisha jibu maswali yafuatayo: -**

Sanaa ni uzuri unaojitokeza katika umbo la kitu. Lakini pia sanaa ni ufundi wowote wa kufanya jambo. Sanaa za Zanzibar ni nyingi. Ukifika Zanzibar utaona sanaa mbalimbali. Ungefika vijijini ungeona watu wakisuka mikoba, mikeka na pakacha. Hiyo inaitwa sanaa ya ususi. Watu hutumia vitu mbali mbali kusuka sanaa hizo. Ukienda katika vijiji vyengine utawaona watu wakicheza ngoma. Sanaa hiyo inaitwa sanaa za ngoma. Ngoma ziko za aina nyingi kama vile ngoma ya beni, msewe, msondo. Watu hutumia ngoma katika sherehe mbali mbali. Wanawake wanapolewa hupigiwa ngoma. Mara nyingi hupigiwa ngoma ya msondo au unyago. Sanaa nyengine ni muziki. Ukifika katika kumbi mbali mbali za burudani utaona muziki wa taarabu, dansi na disko. Sanaa hizi zinapigwa ili watu wafurahi na kushangiria. Pia huwafanya watu waburudike.

Mtu akitembelea Mji mkongwe ataona milango ya nakshi yenye matovu ya chuma. Angalikwenda kwa mafundi seremala angeona makabati, milango na makasha yaliyonakshiwa vizuri. Hizo zote ni kazi za sanaa za ufundi. Sanaa hizo zinazwa kwa bei ya juu na kuwanufaisha wachongaji.

Ungefurahi ungetembelea vijijini katika ukanda wa pwani. Huko ungeona vifaa vya uvuvi vikitengenezwa na wavuvi. Ungeona madema, nyavu, mishipi. Hizi ni sanaa za usukaji. Sanaa hizi zinatumiwa kwa shughuli za uvuvi.

Aidha kuna shughuli za ufuaji wa vyuma. Shughuli hizo ni sanaa za uhunzi. Sanaa hii ni taaluma kongwe sana katika historia ya maisha ya mswahili. Katika sanaa hii watu hupata vifaa mbali mbali kama zana za kilimo; ujenzi, vifaa vya nyumbani, uwindaji, na uvuvi. Miongoni mwa vifaa hivyo ni shoka, panga, mundu, mpae, mtaimbo, mkuki, kisu, majembe, na nyundo. Kwa upande mwingine kuna ufuaji wa dhahabu, fedha na

shaba. Madini haya huyeyushwa na kutengenezwa vitu mbali mbali kama vidani, pete, bangili, herini, vikuku na vipini.

Watu wengi wa Zanzibar wanavaa kofia. Kofia ziko za kazi na ambazo si za kazi. Kofia za kazi hufumwa kwa uzi mzuri. Ukizona utazipenda. Hizi zinatokana na sanaa ya ufumaji. Sanaa nyengine ya Zanzibar ni ufinyanzi. Ufinyanzi unatumia udongo. Vifaa vinavyofinyangwa ni kama vile vyungu, mikungu, na vibia. Vifaa hivi hutumiwa kwa kupikia vyakula na kufunikia.

Ukikutana na kinamama wa Zanzibar utawaona wamechora mikono na miguu. Wanaichora kwa kutumia hina. Ipo pia michoro katika majengo na mabango mbali mbali. Hiyo ni sanaa ya uchoraji. Wachoraji wanatoa huduma katika kuandaa matangazo, mabango ya kutundikwa barabarani, kupamba kumbi na mikutano.

Sanaa za Zanzibar ni muhimu sana katika maisha ya Wazanzibari. Watu wanazitumia katika kukuza uchumi. Sanaa hizi ni sehemu ya utamaduni wa Zanzibar. Vikundi vya sanaa huimarishwa kwa lengo hili.

Sanaa za Zanzibar zimetumika katika kutoa elimu kwa jamii. Walimu hutumia nyimbo katika skuli ili kuwaelimisha mambo mbali mbali kuhusu maisha. Katika siku za hivi karibuni, sanaa ya nyimbo imetumika sana kupiga vita UKIMWI. Vikundi mbali mbali vya sanaa vimeandaliwa ili kuwaelimisha wananchi juu ya madhara ya ugonjwa huo, jinsi ya kujihami na kuwahudumia wagonjwa.

Kwa upande wa uchumi sanaa zinawasaidia watu kupata kipato. Watu huingiza fedha kwa kuuza sanaa zao za uchongaji, uchoraji, uigizaji, usukaji na utarizi. Wasanii wengine hupiga muziki na kujipatia fedha za viingilio. Sanaa za Zanzibar zinafaa kuenziwa. Wasanii wangepewa msaada, ingekuwa jambo zuri. Sanaa zao zingefika mbali sana. Wangukuwa na maisha mazuri kwa sababu ya Sanaa zao.

Zanzibar ni tajiri wa sanaa zote. Sanaa nyingi zilizopo ulimwenguni zinapatikana Zanzibar. Wageni wanapokuja wanazifurahia sanaa za Zanzibar. Watalii hununua sanaa za Zanzibar kama vile michoro, makasha, vilango na vinyago. Sanaa hizo zinapaswa kuimarishwa.

### **Mfano wa Baadhi ya Maswali Yalioulizwa**

- a. Ni sanaa gani zinazoweza kuonekana vijijini?
- b. Unafikiri sanaa za Zanzibar zina umuhimu gani kwa jamii?
- c. Vipi sanaa zinasaidia katika kukuza kipato cha mtu?

Kwa mujibu wa swali hili mtafiti aligundua kwamba, lilikuwa limebeba stadi mbili za lugha stadi ya kusoma na stadi ya kuandika na hizo ndizo hasa stadi ambazo mwanafunzi alifanyiwa upimaji, kwani alitakiwa kuisoma habari baadae ayajibu maswali aliyoulizwa. Kwa mantiki hii mkabala uliotumika wakati wa kutunga maswali ya mtihani huu, ni mkabala unaopima stadi nyingi kwa wakati mmoja ambapo ni moja kati ya misingi ya nadharia ya tabia ya umoja “Unitary Traty Hypothesis” kama ilivyokuwa imeelezwa na kupambanuliwa na nadharia hiyo katika utafiti huu (Oller, 1979).

### **Swali Nambari: 7**

Swali hili lilikuwepo sehemu ya pili ya mtihani huu, swali la saba lilikuwa ni swali la utungaji wa insha, kupitia swali hili mwanafunzi alitakiwa kuchagua mada moja halafu aitungie insha. Swali hilo lilikuwa kama ifuatavyo:-

### **Mfano Nambari: 12**

Tunga insha juu ya mada zifuatazo:-

- i) Maisha yangu juu ya familia za waswahili?
- ii) Wakati gani bora kujifunza lugha za kigeni?
- iii) Matatizo ya vijana duniani
- iv) Eleza utamaduni wa waswahili?

Kupitia swali hili mtafiti aligundua kwamba kwa kiasi kikubwa stadi ya lugha ambayo ilikuwa inapimwa ni stadi ya kuandika, kwani mwanafunzi alitakiwa kuchagua mada

moja akisha aitungie insha. Harmer (2001) anaeleza kwamba hakuna mitihani itakayopima uwezo wa kuandika bila ya kuwemo maswali ya insha. Hata nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Trait Hypothesis) inalitilia mkazo swala hili kwa kusema kwamba wakati wa upimaji wa maswali ya kuandika kuna umuhimu mkubwa wa kuingiza maswali ya insha (Oller 1979).

#### **4.4 Uchambuzi wa Mtihani wa Ana kwa Ana wa Tarehe 30/07/2018**

Mtihani huu ulikuwa na maswali kumi, maswali ambayo yalifanyiwa kazi katika mfumo wa mazugumzo ya mdomo, mwalimu alikuwa analisoma swali moja baada ya jingine huku mwanafunzai anamsikiliza mwalimu katika hali ya ana kwa ana kisha kutoa maelezo au fafanuzi (majibu) kwa njia ya mdomokwa ajili ya kujibu swali husika aliloulizwa. Mfano wa maswali yaliyokuwemo katika mtihani huo ni: -

1. Eleza historia fupi ya maisha yako?
2. Kwa nini unajifunza Kiswahili?
3. Utakaporudi Marekani utaeleza nini kuhusu Zanzibar na utamaduni wa wazanzibari?

Kwa mujibu wa uchambuzi alioufanya mtafiti kupitia mtihani huu wa ana kwa ana wamwaka 2018 Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar katikadarasa la kujifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni la kiwango cha kati. Mtafiti aligundua kwamba stadi za lugha zilizopimwa kupitia mtihani huu ni stadi mbili yaani stadi ya kusikiliza na stadi ya kuzungumza. Hii ni kwa sababu mwalimu alikuwa analisoma swali baada ya hapo mwanafunzi alikuwa anatoa maelezo kwa ajili ya kulijibu swali aliloulizwa.

Kwa hivyo, ilionekana wazi kwamba stadi ya kusikiliza na stadi yakuzungumza zilikuwa zinapimwa sambamba yaani kwa wakati mmoja. Ingawa mtihani wenyewe kiasili uliandaliwa kwa ajili ya kupima stadi ya kuzungumzatu. Heaton (1998) anafafanua katika kitabu chake kinachozungumzia mitihani ya lugha kwa kusema kwamba ubora wa mitihani uko kwenye kile ambacho unasitahiki kukipima na sichengine chochote.

Ikiwa mwalimu anahitaji kupima stadi ya kuzungumzalazima mitihani yake ipime uwezo wa kuzungumza tu, na sio jambo jingine. Nae Brown (2004) kiwango cha ufaulu ambacho kinapatikana katika matokeo ya mitihani lazima kiwe kinaendana, kinaleta mantiki na kinafaida kwa mujibu wa malengo ya mitihani husika. Lakini ukiangalia hapa matokeo yanayopatikana ni tofauti na uasili wa mtihani wenyewe.

Pamoja na hayo, kwa kiasi kikubwa maswali yalioulizwa katika mtihani wa ana kwa ana yalisadifu kufikia malengo ya ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya kigeni kwani wajifunzaji walipimwa kwa mujibu wa mazingira ya matumizi ya lugha lengwa. Kwa uthibitisho wa hilo angalia maswali yalioulizwa katika mtihani huo. Maswali hayo yaliwapa wajifunzaji ujunzi na uzoefu wa kuweza kuitumia lugha kwa mujibu wa mahitaji yao katika maisha ya kila siku.

Kwa upande wa Hancock (2006). Upimaji wa lugha ya kigeni lazima umuwezeshe mjifunzaji kuweza kuitumia lugha katika mahitaji yake ya kila siku kama vile kusikiliza simu, kusoma na kuandika barua pepe kwa watu wao wa karibu. Kwa wajifunzaji wa

lugha ya kigeni kuweza kufikia kiwango hicho cha uelewa ni jambo linalofurahisha zaidi.

Nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Treaty Hypothesis) iliyotumika katika utafiti huu inasisitiza kwamba lugha lazima ipimwe kwa mujibu wa mazingira ya watumiaji. Kwani kuweza kuitumia lugha katika mazingira halisi ya watumiaji ndio msingi mkuu wa kujifunza lugha ya kigeni (Oller, 1979).

Adha, kwa mujibu wa data zilizopatikana kwa njia ya dodoso pamoja na umchambuzi wa nyaraka kupitia mitihani sita ya mwaka 2017, 2018, 2019 mitihani miwili kwa kila mwaka katika fani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni katika kiwango cha kati Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar, kwa kuzingatia maswali mawili kwa kila mtihani ambapo ni swali la kwanza na swali la mwisho, pamoja na mtihani wote wa ana kwa ana wa mwaka 2018.

Matokea ya utafiti huu yalionesha kwamba stadi za lugha zilizokuwa zikipimwa katika mitihani hiyoni zote stadi kuu nne za lugha. Maswali ya ufahamu yaliyokuwemo katika mitihani sita ya kumalizia kozi kupitia swali la kwanza la kila mtihani yalipima stadi mbili kwa wakati mmoja yaani stadi ya kusoma na stadi ya kuandika. Kwa upande wa maswali ya mwisho kwa kila mtihani katika mitihani hiyo yalipima stadi ya kuandika tu, ambapo yalikuwa maswali ya utungaji wa insha. Kwa upande wa maswali yaliyokuwemo katika mtihani wa ana kwa ana yalipima stadi ya kusikiliza na stadi ya kuzungumza. Kwa hivyo matokeo ya utafiti huu yalionesha wazi kwamba mkabala unatumika zaidi katika

utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni chuoni hapo, ni mkabala unaopima stadi nyingi za lugha kwa wakati mmoja (mkabala ujumuishi).

Hali hii ilisisitizwa na nadharia iliyotumika katika utafiti huu pale Oller (1979) aliposema kwamba umahiri wa lugha ni kitu kinachopimwa katika muunganyiko zaidi, kuliko kupimwa katika hali ya kutenganiswa.

#### **4.5 Mtazamo wa Walimu Kuhusu Mkabala Wanaotumia Zaidi**

Kupitia Swali la tatu la utafiti huu, mtafiti alitaka kujua kuhusu mtazamo walionao walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar, juu mkabala wanaotumia zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani chuoni hapo. Katika kulitafutia majibu swali hili mtafiti alitumia mbinu ya dodoso ikiwa ni njia ya ukusanyaji wa data kutoka kwawatoa taarifa.

Kupitia dodoso hili swali la tano lilitumika kwa ajili ya ukamilishaji wa kazi hii. Jadwali lifuatalo litatoa ufafanuzi wa majibu yaliyopatikana kutoka kwa watoa taarifa kwa ajili ya kujibu swali la tatu la utafiti huu kama ifuatavyo: -

### Jadweli 4.3

#### *Mtazamo wa Walimu Kuhusu Mkabala Wanaotumia Zaidi*

**Ufunguo:** Ufafanuzi wa vipengele vya jadweli hili ni sawa sawa na ule uliotolewa katika jadweli la pili hapo juu.

N A	KILICHOPI MWA	USHIRIK I	WALIOJIB U SAHIHI	WASIJIB U SAHIHI	KIWANGO CHA ELIMU			FANI		
					DE G	MAS T	PH D	TEKSO L	ELIM U	KIS W
1	Walimu wanavyouona mkabala unaotumika zaidi	7	5	2	-	5	-	2	1	2

**Chanzo:** Uwandani (Agosti: 2020).

#### 4.5.1 Walimu Wanavyouona Mkabala Unaotumika Zaidi

Katika ukusanyajiwa majibu ya kipengele hiki, ambapo majibu yake yalikusanywa kwa njia ya dodoso kwa kupitia swali lililokuwemo katika dodoso la utafiti huu. Swali pamoja na majibu yake yalikuwa kamaifuatavyo: -

Jee! Unauonaje mkabala unaotumika zaidi katika upimaji wa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni chuoni hapo?

Majibu ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: -

“Ni wenye kufaa kwani unatoa matokeoyanayohitaji katika upimaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni”

Watoa taarifa walionesha uelewa kuhusu kipengele hiki walikuwa watano, wote watano walikuwa na shahada ya uzamili, watoa taarifa wawili walikuwa na shahada ya uzamili



ya ufundishaji Kiswahili kwa wageni, mtoa taarifa mmoja alikuwa na shahada ya uzamili ya elimu na watoa taarifa wawili walikuwa na shahada ya uzamili katika fani ya Kiswahili. Watoa taarifa wawili ambao hawakuonesha uelewa wao kuhusu kipengele hiki mmoja alikuwa na shahada ya uzamili ya Ualimu na mwengine alikuwa na shahada ya uzamili ya Kiswahili.

Kutokana na ufafanuzi huu utafiti ulionyesha kwamba watoa taarifa wenye fani ya ufundishaji Kiswahili kwa wageni na wenye fani ya Kiswahili walikuwa na mtazamo unaofanana juu ya mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kwa wageni. Hughes (1989) anaeleza kwamba mkabala unaopima stadi nyingi za lugha kwa wakati mmoja hutumika katika mitihani ambayo humtaka mtahiniwa kuchanganya vipengele vingi vya lugha kwa wakati mmoja katika kuikamilisha kazi yake.

Alhussain (2009) anaeleza kwamba wanafunzi wanaosomeshwa na kupimwa kwa njia ya mkabala mjumuishi katika lugha ya kigeni hufanikiwa zaidi juu kupata ustadi wa mawasiliano. Kwa upande wa nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Traty Hypothesis) iliyotumika katika utafiti huu inazidi kufafanua kwa kusema kwamba msingi mkuu wa nadharia hii ni kuipima lugha ya kigeni kwa kuzingatia mkabala mjumuishi (Oller 1979).

Aidha, majibu yaliyopatikana katika kulijibu swali la tatu la utafiti huu, majibu ambayo yalichambuliwa kwa njia ya maelezo yalikuwenda sambamba na nadharia ya tabia ya umoja (Unitary Traty Hypothesis) kama ilivyotumika katika utafiti huu pale iliposema kwamba mitihani inayopima stadi mchanganyiko kwa wakati mmoja huipima

lughakatika kiwango kikubwa zaidi na kile kinachopimwa na mkabala unaopima stadi moja kwa wakati mmoja (Oller, 1979).

#### **4.6 Hitimisho**

Kwa ujumla sura hii ilihusika na uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya data ambazo zilipatikana katika utafiti huu, kupitia njia ya dodoso na uchambuzi wa nyaraka kwa lengo la kuweza kuchunguza mkabala wanaoutumia walimu katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Utafiti huu ulikuwa na maswali matatu ambayo yalihitaji kupatiwa majibu kutoka kwa watoa taarifa pamoja na kupata majibu kupitia nyaraka zilizochambuliwa. Kwa hivyo data zilizopatikana kupitia utafiti huu zilisaidia kwa kiwango kikubwa kupata majibu ya utafiti huu, kwa kuzingatia malengomahsusi yaliuongoza utafiti huu kama maelezo yalivyoonekana hapo juu.

## **SURA YA TANO**

### **MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Mtafiti aliigawa Sura hii katika sehemu nne, nazo ni utangulizi, muhutasari wa tasnifu, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

#### **5.2 Muhutasari wa Tasnifu**

Utafiti huu ulikuwa unachunguza mkabala unaotumika katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Huku ukiongozwa na malengo mahsusi matatu, lengo la kwanza lilikuwa kufafanua kwa kiasi gani walimu wanaotunga maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni wanavyoifahamu mikabala ya utungaji mitihani. Pilikubainisha aina ya mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Tatu kufafanua mtazamo wa walimu juu ya mkabala wanaotumia zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

Matokeo ya utafiti huu kwa kila lengo mahsusi yalikuwa kama ifuatavyo: -

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu kupitia lengo la kwanza mtafiti aligundua kwamba, walimu wanaotunga maswali ya mitihani wa Kiswahili kama lugha ya kigeni wanaufahamu wa mikabala ya utungaji mitihani kwa asilimi 57%.

Kwa upande wa matokeo ya lengo la pili la utafiti huu lililochunguza mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Yalionesha wazi kwamba mkabala unatumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni chuoni hapo ni mkabala unaopima stadi nyingi za lugha kwa wakati mmoja.

Aidha, matokeo ya lengo la tatu lililotaka kujua mtazamo wa walimu juu ya mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni yalionesha kwamba, walimu wanaukubali mkabala mchanganyiko kwani unawapatia matokeo wanayoyahitaji katika upimaji.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi matatu, malengo ambayo yaliuongoza utafiti huu kutoka mwanzo hadi mwisho. Pia utafiti huu iliweza kuonesha majibu yaliyopatikana kutokana na kazi nzima kwa kuzingatia malengo mahsusi kama yalivyomuongoza mtafiti wakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Vile vile kutokana na data za utafiti huu, mtafiti alitoa mapendekezo ya ujumla pamoja na mapendekezo ya tafiti zijazo.

### **5.4 Mapendekezo**

Kipengele hiki cha mapendekezo kiligawiwa katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza mapendekezo ya ujumla na sehemu ya pilimapendekezo juu ya tafiti fuatizi.

#### **5.4.1Mapendekezo ya Ujumla**

Mtafiti alipendekeza kwamba ipo haja kwa walimu kufanya jitihada za makusudi juu ya kuongeza taaluma yao katika kipengele cha mikabala ya utungaji wa mitihani, ili wawe na maarifa makubwa zaidi yatakayowasaidia kufahamu kwa upana juu ya upande ambao wanayaegemeza maswali ya mitihani ya Kiswahili kwa wageni wakati wa uandaaji wa mitihani hiyo.

Kwa upande wa Coombe na wenzake (2007) kuna umuhimu na ulazima mkubwa kwa walimu wa lugha ya pili/kigeni kupatiwa mafunzo kuhusu kanuni za msingi zinazohusiana na njia za upimaji wa lugha. Hii ni kwa sababu si walimu wote wanaofundisha lugha ya pili hupata mafunzo rasimini kuhusu upimaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni wanapokuwa masomoni.

Vile vile, ipo haja kwa walimu wanaosomesha Kiswahili kama lugha ya kigeni, kuandaa mazingira yatakayohakikisha kwamba stadi zote kuu nne za lugha, wanazipima kwa wanafunzi wanaowasomesha bila ya kuiacha hata stadi moja, kwani ili mwanafunzi awe mweledi wa lugha fulani ni vizuri kuwa na uwezo wa kutosha katika kuzitumia stadi zote kuu kwa lugha inaohusika husika.

#### **5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti Fuatizi**

Baada ya kukamilika kwa utafiti huu, mtafiti alitoa mapendekezo yafuatayo: -

Kutokana na uchamabuzi wa data na matokeo yaliopatikana kupitia data hizo, utafiti huu utakuwa ni muanga wa kutafakari na kuona nini cha kufanya katika ulimwengu huu wa

kitaaluma. Kama mtafiti alivyosema hapo awali kwamba, utafiti huu ulichunguza mkabala unaotumikakatika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni katika kiwango cha kati.

Kwa hivyo, ipo haja kwa watafiti wengine kufanya utafiti katika kiwango cha chini na kiwango cha juu, kuhusu aina ya mikabala inayotumika katika utungaji wa maswali ya mitihani ya Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Vile vile, ipo haja ya kufanya utafiti juu ya kuchunguzastadi nyingine za lugha kama sarufi, msamiati, matamshi katika ufundishwaji na upimwaji wake kwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili kama lugha ya kigeni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar.

## MAREJEO

- Addo, M. and Eboh, W. (2014). *Qualitative Vs quantitative research methods*. Publisher: Sage Publications.
- Alhussain, A. (2009). *Proposing and testing an integrative approach to improve EFL students' communicative*. Princess Nora Bint Abdul Rahman University
- Bachman. (1991). *What does language testing have to offer?* Published by: Teachers of English to Speakers of Other Languages (TESOL)
- Bachman, L. F. (1995). *Fundamental consideration in language Testing*. Oxford University Press.
- Bachman, L.F. and Palmer, A.S. (1996). *Developing effective assessment in higher education: A Practical Guide*. Maidenhead. Oxford University Press.
- Bachman L F (2010). *Second language assessment*. In: Penelope Peterson, Eva Baker, Barry McGaw, (Editors), *International Encyclopedia of Education*. Volume4, pp. 140-147. Elsevier.
- Bell, R. T. (1981). *An introduction to applied linguistics: Approaches and Methodology language leaching*. St. Martin's Press
- Brown, H.D. (2004). *Language assessment: Principles and classroom practices*. Pearson education Press.
- Carroll, J. B. (1961). *Fundamental considerations in testing for English language proficiency of foreign students*. Testing. Center for Applied Linguistics.
- Carroll, J. B. (1968). *The psychology of language testing*. In A. Davies (ed.), *Language testing symposium: A psycholinguistic approach* (pp. 46–69). Oxford University Press.
- Canale, M. & Swain, M. (1980). *Theoretical bases of communicative approaches to second language teaching and testing*. *Applied Linguistics*, 1(1), 1–47.
- Cohen, A. (1994). *Assessing language ability in the classroom*. Heinle and Heinle.
- Coombe, C., Folse, K. & Hubley, N. (2007). *A practical guide to assessing English language learners*. University of Michigan Press

- Das, T.H (1983). *Qualitative research in organizational behavior*. Journal of Management studies vol.20 no 3, p311<https://doi.org/10.1111/j.1467-6486.1983.tb00209>.
- Giraldo, F. (2018). *Language assessment literacy: Implications for language teachers*. Profile: Issues in Teachers' Professional Development, 20(1), 179-195. <https://doi.org/10.15446/profile.v20n1.62089>
- Hancock. C (2006). *Language teaching and language testing: a way and ways to make appropriate connections*. The Ohio State University
- Harris, D. (1969). *Testing English as a second language*. Publisher McGraw Hill.
- Heaton, J.B. (1990). *Class room testing*. Longman Press.
- Hossan. (2015). *Is grading system important*. <http://blogs.It.vt.edu/hossam/2015.07/01/2020>
- Holland, K. and Rees, C (2010) *Evidence- based practice skill*. Oxford University Press
- Hughes, N. (1989). *Testing for language teachers*. Cambridge University Press
- Lado, R. (1961). *Language Testing: The Construction and Use of Foreign Language Test*. Longman.Green and Company
- López, A. and Bernal, R. (2009). *Language Testing in Colombia: A call for more teacher education and teacher training in language assessment*. Profile: Issues in Teachers' Professional Development, 11(2), 55-70.
- Lundahl, C. (2014) *Bedömning*. I U. P. Lundgren, R. Säljö & C. Liberg (red.), *Lärande Skola Bildning* (s. 519-557). Stockholm: Natur & Kultur.
- Magno, C. (2010). *The function of grading students*. De La Salle University Press
- Miles, M.B. and Huberman, A.M. (1994). *Qualitative data analysis*. SAGE, International Education and Professional Publisher.
- Moeller.A. K and Catalano, T. (2015). *Foreign language teaching and learning*. Faculty Publications: Department of Teaching, Learning and Teacher Education. 200.
- Oller, J. W. (1979). *Languahe tests at school: A pragmatic approach*. Printed in Great Britain by Butler Tanner Ltd.



- Oller, J. W. (1973). *Pragmatic perspectives for the language teacher*. Publisher: Newbury House.
- Oller, J. W. and Richards J. (1973). “*Discrete Point Tests Versus Tests of Intergrative Skills*”. J W Oller & J.C. Richards (eds.) Focus on Learner. Massachusetts: Newbury House,
- Oller, J. W (1986). *Communicative competence: Theory and classroom Practice*. Reading, MA: Addison-Wesley Second Language Professional Library Series.
- Pacitti, B.J. (1998), Organisational learning in R&D organisations: a study of new product development projects, unpublished PhD thesis, University of Manchester,
- Punch, K. F. and Punch (2005). *Introduction to Social Research—Quantitative & Qualitative Approaches*. Sage.
- Ramadan, M. (2020). *English language teaching and test*. Guide [www:/elttguide.com/12-Characteristics](http://www:/elttguide.com/12-Characteristics) 15 January 2020.
- Roopa, S. and Rani, MS. (2012). *Questionnaire designing for a survey*. J Ind Orthod. SOC; 46(4):2730-277.
- Spolsky B. (1975). *Language testing: Art or science*” A paper presented at the fourth AILA international congress.
- Stake, R. (2006). *Multiple case study analysis*. Guilford Press.
- Tran, T. (2012). *Second language assessment for classroom teachers*. Missouri University of Science and Technology. Paper Presented at MIDTESOL 2012, Ames, Iowa
- Tromp, D. Kombo. (2006). *Proposal & thesis writing: An introduction*. Paulines Publications Africa
- Yin, R. (2003). *Case study reserarch: Design and methods*. (3rd ed). SAGE; Publication Thousand Oaks,

**KIAMBATISHO 1: DODOSO LA UTAFITI**

**MKABALA UNAOTUMIKA KATIKA UTUNGAJI WA MITIHANI YA  
KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI:**

**Mfano Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar**

**UTANGULIZI**

Dodoso hili limeandaliwa ili kuchunguza mkabala unaotumika zaidi katika utungaji wa maswali ya mitihani ya mwisho ya Kiswahili kwa wageni katika kiwango cha kati ya mwaka 2017, 2018 na 2019 Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar. Unaombwa ushiriki katika ujazaji wa dodoso hili, majibu ya dodoso hili yatakua ni siri baina yako na mtafiti na wala hayatotumika kinyume na malengo ya utafiti huu. Ujazaji wa dodoso hili ni wa hiyari na pindipo ukikutana na swali ambalo unahizi unahitaji ufafanuzi wa ziada mtafiti atakupatia, pia uko huru kuendelea kuwa mtoa taarifa wa utafiti huu au kujitoa wakati wowote. Kwa ajili ya mawasiliano na mtafiti +255 776 583466

**MAELEZO BINAFSI YA MTOA TAARIFA**

Kiwango cha elimu..... Uzoefu wa kazi .....

Aina ya digrii..... Jinsi.....

1. Nini maana ya mikabala ya utungaji mitihani ya lugha?

.....  
.....

2. a) Kuna aina ngapi za mikabala ya utungaji wa mitihani ya lugha?

.....  
.....

b) Zitaje

.....

3. Mkabala unaopima stadi moja ya lugha kwa wakati mmoja unawiyana vipi na mkabala unaopima stadi mchanganyiko?

.....  
.....

4. Bainisha mkabala unaotumitua zaidi katika utungaji wa mitihani ya Kiswahili kwa wageni Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar?

.....

5. Jee! Unauonaje mkabala unaotumika zaidi katika upimaji wa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni chuoni hapo?

.....

**KIAMBATISHO 2: MTIHANI WA KIWANGO CHA**

**KATI WA TAREHE 29/09/2017**

**CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR  
SKULI YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIGENI  
IDARA YA KISWAHILI KWA WAGENI (SUZA)**

**MTIHANI WA MWISHO**

**KIWANGO CHA KATI**

**JINA: .....29/09/2017**

**1. Soma ufahamu na baadae ujibu maswali yanayofuata chini**

Mfumo wa maisha ya jamii hivi sasa ni mfumo unaotawaliwa kwa kiasi kikubwa na matumizi ya fedha. Namna mojawapo ya wanajamii kupata fedha ni kupitia kuajiriwa. Zipo ajira rasmi na ajira zisizo rasmi. Ajira rasmi ni kama vile uaskari, udaktari, ualimu, udereva. Ajira zisizo rasmi ni kama vile uuzaji wa matunda na mboga mboga, uendeshaji wa duka au mkahawa, kufanya vibarua mashambani na ushonaji.

Mfumo huu wa maisha umesababisha si tu watu wazima kufanya kazi hizo mbali mbali ili kujipatia fedha, bali pia watoto wengi wameingizwa kwenye ajira, hasa katika mfumo wa ajira zisizo rasmi. Watoto wengi wanafanya kazi kwenye migodi, kama vile ya dhahabu na tanzanaiti; kwenye mashamba, kama vile ya chai, kahawa na pamba; kwenye kazi za majumbani, kama vile kulima, kufua, kupika na kuchunga mifugo; kwenye upasuaji wa mbao n.k.

Ziko hasara nyingi zinazotokana na kitendo cha kuajiri watoto. Kukosa fursa ya kupata elimu ni hasara mojawapo kubwa. Wapo watoto wengi ambao wameacha shule ili waweze kwenda kufanya kazi za kuajiriwa. Hasara nyingine ni kuathirika kwa ukuaji wao. Kuna watoto wengi ambao umri wao ni mdogo, lakini wanafanyishwa kazi nzito mno. Kazi hizo ni kama vile kupasua mbao, kuvunja kokoto na kuvunja mawe yenye madini migodini. Hizi ni kazi ambazo haziendani na umri wao, hivyo huelemea miili yao ambayo bado ni michanga na kuifanya isikue sawasawa.

Vilevile watoto wengi hudhulumiwa hata kiasi kile kidogo cha malipo ambacho waliahidiwa kulipwa na hao waajiri wao. Pale wanapodai malipo yao, hufukuzwa. Hatima yake ni kukosa namna ya kujikimu kimaisha, hivyo kujiingiza katika makundi

ya watoto wa mitaani na kuanza kutumia dawa za kulevya na hata kufanya ukahaba. Hasara nyingine ni kutengwa na familia zao, mathalani hutolewa vijijini na kupelekwa mijini, watoto hao hukosa malezi ya wazazi, hivyo hutumbukia kirahisi katika makundi ya kihalifu, kama vile ujambazi na uvutaji bangi.

